SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

MKAKATI WA KUIMARISHA UTAWALA NA UONGOZI WA UVUVI ZANZIBAR

JUNI 2014

SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

MKAKATI WA KUIMARISHA UTAWALA NA UONGOZI WA UVUVI ZANZIBAR

JUNI 2014

VIFUPISHO

CHABAMKA	Changu-Bawe Conservation Area – Eneo la Hifadhi la Changu na Bawe
DFD	Department of Fisheries Development – Idara ya Maendeleo ya Uvuvi
DFO	District Fisheries Officer – Afisa Uvuvi wa Wilaya
DMR	Department of Marine Resources – Idara ya Rasilimali za Baharini
DSFA	Deep Sea Fishing Authority – Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu
EEZ	Exclusive Economic Zone – Ukanda Maalumu wa Kiuchumi
ESA - IO	Eastern Southern Afrika – Indian Ocean – Bahari ya Hindi ya Kusini Mashariki ya Afrika
EU	European Union – Umoja wa Ulaya
FAD	Fish Aggregating Devices - Maumbo Yanayowavutia Samaki
FAO	Food and Agriculture Organization of United Nations – Shirika la Chakula na Kilimo Dunia
FETA	Fisheries Education and Training – Shirika la Mafunzo na Uwakala wa Uvuvi
FMP	Fisheries Management Plans (for MCA) – Mipango ya Usimamizi wa Uvuvi (kwa Maeneo ya Hifadhi ya Bahari)
GDP	Gross Domestic Product – Pato la Ndani la Taifa
GMP	General Management Plan (for MCA) – Mpango Mkuu wa Usimamizi wa Uvuvi (kwa Maeneo ya Hifadhi ya Bahari)
ICZM	Intergrated Coastal Zone Management – Usimamizi Shirikishi wa Ukanda wa Pwani
IOC	Indian Ocean Commission – Kamisheni ya Bahari ya Hindi
IOTC	Indian Ocean Tuna Commission – Kamisheni ya Tuna ya Bahari ya Hindi
IMS	Institute of Marine Science – Taasisi ya Sayansi za Bahari
IUU	Illegal, Unreported and Unregulated Fishing - Uvuvi Haramu, Usiofahamika na Usiofuata Kanuni
KMKM	Zanzibar Navy – Kikosi Maalumu cha Kuzuia Magendo
MACEMP	Marine and Coastal Environment Management Project - Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na Pwani
MBCA	Menai Bay Conservation Area – Eneo la Hifadhi ya Ghuba ya Minai
MCA	Marine Conservation Area – Maeneo ya Hifadhi ya Bahari
MCS	Minitoring, Control and Surveillance – Ufuatiliaji, Udhibiti na Ulinzi
MCU	Marine Conservation Unit – Kitengo cha Hifadhi ya Bahari
MIMCA	Mnemba Island-Chwaka Bay Conservation Area – Eneo la Hifadhi ya Kisiwa cha Mnemba na Ghuba ya Chwaka
MKUZA II	Zanzibar Strategy for Growth and Reduction of Poverty 2010 - 2015 – Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar Sehemu ya Pili - 2010 - 2015

MLF	Ministry of Livestock and Fisheries – Wizara ya Mifugo na Uvuvi (WMU)
MSY	Maximum Sustainable Yield – Kiwango cha Juu kinachoendeleza Uzalishaji
NGO	Non Governmental Organization –Mashirika yasiyo ya Kiserikali
PeCCA	Pemba Channel Concervation Area - Hifadhi ya Bahari ya Mkondo wa Pemba
PSE	Priority Regulation for Strong Enforcement - Kanuni ya Kipaumbele cha Kusimamia sheria ipasavyo
SUZA	The State Univsersity of Zanzibar – Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar
SWIOFish	South West Indian Ocean Fisheries Governance and Shared Growth Programme – Programu ya Shirikishi ya Utawala na Uendelezaji wa Uvuvi Kusini Magharibi ya Bahari ya Hindi
SWIOFP	South West Indian Ocean Fisheries Programme – Programu ya Uvuvi Kusini Magharibi ya Bahari ya Hindi
TAFIRI	Tanzania Fisheries Research Institute - Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania
TUMCA	Tumbatu Marine Conservation Area – Eneo la Hifadhi ya Bahari ya Tumbatu
VFC	Village Fishing Communities – Kamati za Uvuvi za Vijiji
Vision 2020	Zanzibar Development Vision, 2020 – Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar wa 2020
VSFC	Village Seaweed Fishing Commitees - Kamati za Mwani za Vijiji
WIOMSA	West Indian Ocean Marine Science Association – Jumuiya ya Sayansi ya Bahari ya Magharibi ya Bahari ya Hindi
ZAMP	Zanzibar Agricultural Marketing Policy – Sera ya Masoko ya Bidhaa za Kilimo Zanzibar
ZMA	Zanzibar Maritime Authority – Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar
ZU	Zanzibar University – Chuo Kikuu cha Zanzibar

YALIYOMO

VIFUPISHO **1**

YALIYOMO **3**

DIBAJI **6**

1. UTANGULIZI **7**

2. UMUHIMU WA KUWA NA MKAKATI WA UONGOZI WA UVUVI **9**

2.1 DHANA MUHIMU ZINAZOHUSIANA NA UTAWALA WA UVUVI 9

2.2 KAZI NA NAFASI YA MKAKATI WA UTAWALA WA UVUVI KATIKA UTAWALA NA USIMAMIZI WA UVUVI 11

2.3 MAMBO MUHIMU YA KISEKTA YATAKAYOZINGATIWA KATIKA MKAKATI WA UTAWALA WA UVUVI. 12

2.3.1 HATUA ILIYOPIGWA NA SEKTA YA UVUVI KWA MUJIBU WA MALENGO YA VISION 2020 NA MKUZA II 13

2.3.2 UPUNGUFU NA UDHAIFU MKUU KATIKA MFUMO WA SASA WA UTAWALA ..... …16

2.3.3 UBORA NA FURSA ZILIZOMO KWENYE MFUMO WA UTALAWA 18

3. MALENGO NA MISINGI ELEKEZI YA MKAKATI WA UTAWALA WA UVUVI **20**

3.1 MALENGO YA MKAKATI WA UTAWALA WA UVUVI 20

3.2 MISINGI ELEKEZI MIKUU 20

3.2.1 USIMAMIZI WA UVUVI WA KARIBU NA PWANI 20

3.2.2 MAENDELEO YA UVUVI MBALI NA FUKWE KWENYE BAHARI KUU 23

3.2.3 KUONGEZA THAMANI KATIKA UVUVI 26

3.2.4 MAMBO MENGINE YANAYOPASWA KUIMARISHA KATIKA MFUMO WA UTAWALA ILI KUUFANYA UJITOSHELEZE KWA AJILI KULETA “HALI BORA ZAIDI” KATIKA USIMAMIZI \WA SEKTA YA UVUV 27

4. VIPENGELE VYA KIMKAKATI VYA KUIMARISHA UTAWALA NA USIMAMIZI WA UVUVI ZANZIBAR **28**

4.1 KUIMARISHA VIPENGELE MUHIMU KATIKA MHIMILI WA UTAWALA WA UVUVI..... 28

4.1.1 KUIPITIA NA KUIBADILISHA SERA YA UVUVI YA MWAKA 2000 28

4.1.2 KUSHAJIISHA UKAMILISHAJI NA UPITISHAJI WA VIFUNGU VYA SHERIA YA UVUVI YA MWAKA 2010 VINAVYOSAIDIA UTEKELEZAJI WA MKAKATI 28

4.1.3 KUIMARISHA UFANISI WA UONGOZI WA UVUVI 29
4.1.4 KUJENGA UWEZO KWA ASASI ZA UVUVI ZA KIJAMII NA BINAFSI 30
4.1.5 KUIMARISHA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA, KIKANDA NA KITAIFA KATIKA SEKTA YA UVUVI 30
4.1.6 KUFANYIA MABADILIKO SHERIA YA UVUVI YA MWAKA 2010 ILI IIMARISHE UTAWALA WA UVUVI (MTAZAMO WA MUDA WA KATI HADI MUDA MREFU) 31
4.2 KUIMARISHA UTOAJI WA HUDUMA MUHIMU ZA UVUVI 32
4.2.1 KUFANYIA MAREKEBISHO MFUMO WA TAKWIMU NA UTOAJI TAARIFA 32
4.2.2 KUENDELEA KUIMARISHA UDHIBITI NA ULINZI KATIKA UVUVI 32
4.2.3 KUWEKA MFUMO BORA WA UTAFITI WA UVUVI 33
4.2.4 KUANDAA MFUMO WA TAARIFA ZA UVUVI 35
4.2.5 UFUATILIAJI NA TATHMINI YA MKAKATI WA UTAWALA WA UVUVI 36
4.3 KUZIFANYA SHUGHULI ZA UVUVI NA NYENGINE ZINAZOLINGANA NA UVUVI KUWA RASMI NA ZA KITAALAMU 36
4.3.1 KUWEKA MASHARTI YA CHINI YA KURUHUSIWA KUVUA 36
4.3.2 KUKAMILISHA NA KUTEKELEZA BANDARI RASMI ZA UVUVI 37
4.3.3 KUIMARISHA MIKAKATI YA KUNYANYUA HALI ZA MAISHA ZA JAMII ZA WAVUVI (KWA KUTOA KIPAUMBELE KWA KIZAZI KIPYA) 37
4.4 KUIMARISHA USIMAMIZI WA UVUVI WA MAENEO YA BAHARI YA KARIBU NA PWANI 38
4.4.1 KUIMARISHA UFANYAJI KAZI NA USIMAMIZI WA MAENEO YA HIFADHI YA BAHARI (MCAs) 38
4.4.2 KUIMARISHA MBINU YA KANUNI YA KIPAUMBELE CHA KUSIMAMIA SHERIA IPASAVYO (PRIORITY REGULATION FOR STRONG ENFORCEMENT – PSE) KWA UVUVI WA BAHARI YA KARIBU YA PWANI NJE YA MAENEO YA HIFADHI YA BAHARI 39
4.4.3 KUIMARISHA MIPANGO YA USIMAMIZI WA UVUVI (FISHERIES MANAGEMENT PLANS – FMPs) KATIKA AINA ZA UVUVI ZINAZOPEWA KIPAUMBELE 40
4.4.4 KUENDELEZA UTEKELEZAJI WA MIPANGO YA UHIFADHI WA MAZINGIRA YA MAENEO YA PWANI (ICMZ) 42
4.4.5 KUIMARISHA MFUMO WA KITAIFA WA KUZUIA NA KUPAMBANA NA UCHAFUZI WA MAZINGIRA YA BAHARI 43

4.4.6 KUIMARISHA USIMAMIZI WA UVUVI WA BAHARI YA KARIBU NA PWANI KATIKA MPANGO WA MUDA WA KATI MPAKA MUDA MREFU 43
4.5 KUENDELEZA UVUVI WABAHARI KUU 44
4.5.1 KUENDELEZA MATAYARISHO NA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU YA KUANZISHA NA KUSIMAMIA UVUVI WA FAD 44
4.5.2 KUIMARISHA UFANISI NA USALAMA WA VYOMBO VYA UVUVI KATIKA BAHARI KUU 46
4.6 KUIMARISHA MAENDELEO YA KILIMO CHA BAHARINI KINACHOZINGATIA UHIFADHI WA MAZINGIRA 46
4.6.1 KUENDELEZA KILIMO CHA MWANI 46
4.6.2 KUIMARISHA MATAYARISHO NA UTEKELEZAJI WA MPANGO MKAKATI WA KILIMO CHA BAHARINI ZANZIBAR. 46
4.7 KUIMARISHA ONGEZEKO LA THAMANI NA KUSAIDIA KUPUNGUZA UMASIKINI KATIKA SEKTA YA BAADA YA MAVUNO 47
4.7.1 KUONGEZA UBORA WA SAMAKI PAMOJA NA KUPUNGUZA UPOTEVU WA SAMAKI NA HASARA YA KIUCHUMI 48
4.7.2 KUONGEZA THAMANI KATIKA UVUVI (MUDA WA KATI HADI MREFU) 48
5. UTEKELEZAJI WAMKAKATI WA UTAWALA WA UVUVI 49
5.1 UFUPISHO WA MIONGOZO YA UTEKELEZAJI KWA AJILI YA KUIMARISHA UTAWALA NA USIMAMIZI WA UVUVI PAMONA NA HATUA ZINAZOPEWA KIPAUMBELE 49
5.2 BAADHI YA MISINGI ELEKEZI YA UTEKELEZAJI WA MKAKATI WA UTAWALA WA UVUVI 49
6. **KIAMBATISHO: BANGO KITITA LA MKAKATI WA KUIMARISHA UTAWALA NA USIMAMIZI WA UVUVI ZANZIBAR 52**

DIBAJI

Wizara ya Mifugo na Uvuvi, tokea July 2013, imekuwa ikitayarisha Mkakati wa Kuimarisha Utawala na Uongozi wa Uvuvi Zanzibar (Utakaojulikana kama Mkakati wa Utawala wa Uvuvi). Mkakati huu unafadhiliwa na Umoja wa Ulaya kupitia Programu ya Smartfish.

Utayarishaji wa Mkakati huu umepita katika hatua mbali mbali, ikiwemo kufanyika kwa warsha mbali mbali zilizowashirikisha wadau wa sekta ya uvuvi. Matokeo ya warsha hizo ni kuandaliwa kwa Mswada wa Mkakati wa Utawala wa Uvuvi mwezi Machi 2014. Mkutano maalumu wa Kamati ya Wataalamu ya Waziri uliitishwa tarehe 15 Mei 2014 kwa lengo la kuupitia Mswada huo. Kamati hiyo iliongozwa na Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo na Uvuvi.

Kamati ya Wataalamu iliukubali Mkakati huo kwamba unafaa lakini kwa sharti ya kwanza kuingizwa kwa mapendekezo kadhaa yaliyotolewa na Kamati hiyo.

Mkakati huu tayari umeyaingiza mapendekezo yote yaliyotolewa na Kamati ya Wataalamu ya Waziri na kuwa tolea jipya ukulinganisha na lile la awali lililopelekwa kwenye Kamati hiyo. Toleo hili na hatua nyengine muhimu miongoni mwa hatua rasmi za kuelekea kupatikana kwa Mkakati wa Utawala wa Uvuvi. Hatua zitakazofuata ni kupelekwa kwa Mswada huu kwenye Kamati ya Wataalamu kutoka Wizara mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na hatimaye kuwasilishwa katika Baraza la Mawaziri.

1. UTANGULIZI

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeundwa na Tanzania Bara na Zanzibar. Zanzibar ni mkusanyiko wa Visiwa vikuu viwili vya Unguja na Pemba pamoja na visiwa vyengine vidogo vidogo vinavyofikia 50. Katika muundo wa Muungano, Zanzibar ina mamlaka kamili ya usimamizi wa shughuli za uvuvi zinazofanyika katika eneo lake la bahari (ambalo ni maili 12 kwa vipimo vya kibaharia) pamoja na eneo ndani la bahari (ambalo ni kuanzia ufukweni hadi kati kati ya bahari baina ya Tanzania Bara na Zanzibar). Uvuvi unaofanyika katika eneo la Bahari ya Zanzibar pamoja na eneo la ndani la bahari unasimamiwa na Idara zinazohusika na Uvuvi na Kilimo cha baharini za Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya Zanzibar. Idara hizo ni Idara ya Maendeleo ya Uvuvi (IMU) na Idara ya Rasilimali za Baharini (IRB). Katika maandiko haya, dhana ya “Usimamizi wa Uvuvi” utazijumuisha idara zote mbili ili kurahisisha usomaji.

Kwa kuzingatia umuhimu wa sekta ya uvuvi kwa uchumi wa Zanzibar, Wizara inayohusika na masuala ya uvuvi imekuwa ikisaidia kila hatua inayochukuliwa katika uimarisha wa uvuvi unaokubalika na endelevu. Hatua hizo ni pamoja na kupitishwa kwa Sheria mpya ya Uvuvi ya mwaka 2010, Kurekebisha muundo wa usimamizi wa uvuvi katika mwaka huo huo, kuanzishwa kwa Kitengo cha Uhifadhi wa Bahari (KUB), kuanzishwa kwa kanuni zinazoimarisha utawala wa Udhibiti wa Maeneo ya Bahari, na kuandaa Mipango Mikuu ya Usimamizi wa kila Eneo la Hifadhi ya Bahari. Hatua nyengine ni kuimarisha udhibiti na ukaguzi wa shughuli za uvuvi hasa katika Maeneo ya Hifadhi, kuimarisha ushirikishwaji wa jamii za wavuvi katika usimamizi wa uvuvi kwa njia ya uanzishaji wa Kamati za Uvuvi za Vijiji na kuandaa mpango wa ushirikiano na taasisi nyengine ili kusaidia utekelezaji wa Usimamizi Shirikishi wa Maeneo ya Mwambao.

Hata hivyo, sekta ya uvuvi inakabiliwa na changamoto kadhaa ambazo kwa kiasi kikubwa huathiri upatikanaji endelevu wa rasilimali za samaki katika sehemu zenye kina kifupi cha maji. Kutokana na hali hiyo, sekta hii inashindwa kuchangia ipasavyo maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya Zanzibar. Aidha, namna shughuli za uvuvi zinavyofanyika kwa sasa zinashindwa kuchangia kufikiwa kwa malengo yaliyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar wa 2020 (Vision 2020) na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar Sehemu ya Pili (MKUZA II) ambayo yanalenga kuhakikisha kwamba kuna usimamizi endelevu wa uvuvi wa karibu na pwani, kusaidia uhifadhi wa utajiri wa mfumo wa ikolojia wa miamba wa Zanzibar na kuendeleza uvuvi wa mkondoni ambako rasilimali za uvuvi hazitumika ipasavyo.

Katika kushughulikia changamoto hizo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi hivi karibuni ilianzisha utaratibu wa kuifanyia marekebisho Sera ya Uvuvi ya mwaka 2000 ambayo imepitwa na wakati. Wizara pia inaandaa Mradi wa Uvuvi unaotazamiwa kuleta tija zaidi kwa ufadhili wa mpango maalumu wa kikanda wa Benki ya Dunia unaojulikana kama Programu ya SWIOFish (SWIOFish Programme).

Wizara inayoshughulikia mifugo na Uvuvi pia imeiomba programu inayofadhiliwa na Jumuiya ya Ulaya, SmartFish, kusaidia katika kuandaa Mkakati wa kuimarisha utawala na usimamizi wa Uvuvi Zanzibar (ambao utaitwa ‘Mkakati wa Utawala wa Uvuvi’). Lengo kuu la Mkakati wa Utawala wa Uvuvi ni kuweka kanuni elekezi zitakazozingatia kujumuisha kanuni za utawala bora katika usimamizi wa sekta ya uvuvi na kupendekeza mpango rasmi wa kuimarisha mfumo wa sasa wa uvuvi. Lengo la mipango hii ni kuiwezesha sekta ya utalii kuchangia kwa kiwango kikubwa zaidi katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi Zanzibar kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar wa 2020 (Vision 2020) na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar Sehemu ya Pili (MKUZA II)

Mkakati wa Utawala wa Uvuvi unasisitiza ushirikishwaji wa Taasisi mbali mbali za serikali na binafsi ambazo zinahusiana na masuala ya uvuvi moja kwa moja au kwa njia nyengine yoyote ile katika Uongozi wa Uvuvi. Mkakati utakuwa kiongozi kikuu cha utekelezaji na ufuatiliji wa shughuli za Uvuvi.

Ni kutokana na muktadha huo, kwamba Programu ya SmartFish imetoa msaada wa muda wa kuunda

Mkakati huu kwa Wizara inayoshughulikia uvuvi kuanzia Julai 2013. Mchakato wa uundaji wa Mkakati wa Uongozi wa Uvuvi umejumuisha kufanyika kwa uchunguzi wa kina kuhusu matatizo yaliyomo katika sekta ya uvuvi ulifanywa na mshauri mwelekezi wa kimataifa kwa kushirikiana na kamisheni mbili za kitaalamu. Mchakato pia ulijumuisha warsha ya wadau mbali mbali wa uvuvi iliyofanyika Pemba Desemba mwaka 2013. Warsha hiyo ilichangia mawazo kadhaa muhimu ambayo yalisaidia katika uandaaji wa muswada wa Mkakati wa Uongozi wa wa Uvuvi. Ripoti ya Uchunguzi wa Hali ya Uvuvi Zanzibar imechapishwa na SmartFish kama maandiko mbali na Mkakati huu[1] .

Mchakato wa kuandaa Mkakati wa Uongozi pia umepitia hatua ya kufanya warsha nyengine ya wadau mbali mbali wa uvuvi iliyofanyika Mji Mkongwe katikati ya mwezi Machi mwaka 2014. Lengo la warsha hiyo ilikuwa ni kujadili na kufafanua zaidi Toleo la Awali la Mkakati wa Uongozi wa Uvuvi. Matokeo ya warsha hiyo yapelekea kupatikana kwa Mkakati wa Uongozi na Usimamizi wa Uvuvi Zanzibar ambao ulikuwa ni uimarishaji wa Toleo la awali. Mkakati huu mpya uliandaliwa na Mshauri Mwelekezi kutoka SmartFish na kusambazwa katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Toleo la Mwisho la Mkakati wa Utawala na Usimamizi wa Uvuvi lilipitiwa na Kamati ya Wataalamu ya Wizara (MTC) ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi tarehe 15 Mei 2014, ambayo iliuidhinisha Mkakati huo kwa sharti la kwanza kuingizwa kwa baadhi ya mapendekezo yaliyotolewa na Kamati hiyo.

Mkakati huu tayari umeyaingiza mapendekezo yote yaliyotolewa na Kamati ya Wataalamu ya Waziri na kuwa tolea jipya ukulinganisha na lile la awali lililopelekwa kwenye Kamati hiyo. Hatua zitakazofuata ni kupelekwa kwa Mswada huu kwenye Kamati ya Wataalamu kutoka Wizara mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na hatimaye kuwasilishwa katika Baraza la Mawaziri.

Katika hatua za mwisho, Programu ya SmartFish inatarajia kuisaidia Wizara inayoshughulikia uvuvi kuandaa hafla ya kuutangaza Mkakati wa Utawala wa Uvuvi baada ya Toleo la Mwisho la Mkakati huu kukubaliwa na kuidhinishwa na Baraza la Mawaziri. Kwa sasa, Programu ya SmartFish inasaidia katika kuhakikisha kwamba kunakuwa na uwiyano baina na Mkakati wa Utawala wa Uvuvi na Sera ya Uvuvi ya mwaka 2000 ambayo imo katika mchakato wa kupitiwa, kufanyiwa mabadiliko na kuimarishwa zaidi. Sera mpya ya Uvuvi itakayokuja itachukuliwa kama kitendea kazi kikubwa cha kisera kitakachoongoza utekelezaji wa Mkakati wa Utawala wa Uvuvi kama itakavyofafanuliwa zaidi hapo chini.

2. UMUHIMU WA KUWA NA MKAKATI WA UONGOZI WA UVUVI.

2.1 DHANA MUHIMU ZINAZOHUSIANA NA UTAWALA WA UVUVI

Kwa lugha nyepesi kabisa, Utawala ni namna ya kuongoza. Kwa maneno mengine, utawala bora ni kuongoza vizuri, wakati kuongoza vizuri ni hali ya kuzingatia mawazo ya watu na imani za kijamii na kiutamaduni katika uongozi. Mawazo na imani hizo mara nyingi hutafautiana kati ya nchi na nchi.

Hata hivyo, dhana inayokubalika kimataifa kuhusiana na utawala bora ni kuunda dola bora ambalo litasimamia utoaji wa huduma kwa jamii kwa ufanisi na kwa kuzingatia matakwa ya wengi. Dhana hii ya “Dola Bora” katika kutekeleza shughuli za utawala (kinyume na ‘Dola

Peke Yake’ na ‘Bila ya Dola’) ni michakato inayoongozwa na misingi kadhaa ya uadilifu kama vile upatikanaji wa taarifa, mashauriano na watumiaji, ushirikiano kati ya serikali na sekta binafsi katika utoaji wa baadhi ya huduma, ufanisi katika huduma za jamii n.k.

Kwa hivyo, kushughulikia suala la utawala ni sawa na kutilia mkazo namna huduma za jamii zinavyopangwa na kutekelezwa, pia inaonesha kutilia mkazo ubora wa huduma za jamii (kwa mujibu wa mshikamamo na uthabiti wa huduma).

1 Breuli, C (2014) Diagnosis-Analysis of Fishery Sector in Zanzibar. SmartFish Programme.

Dhana ya utawala bora inatajwa mara kwa mara katika usimamizi wa sekta ya uvuvi kama mojawapo ya masharti yanayosababisha kufikiwa kwa malengo ya kuwa na uvuvi endelevu na unaozingatia uhifadhi wa mazingira.

Ikumbukwe pia kwamba rasilimali zinazotokana na uvuvi ni rasilimali zinazorejesheka ambazo mara nyingi kupatikana kwake hutegemea kutolewa kwa ruhusa ya mtu binafsi kumiliki. Lengo kuu la kumiliki huku ni kuongeza tija, kutengeneza fursa za ajira/kusaidia katika upatikanaji ya mahitaji ya lazima ya kila siku. Namna haki hizi zilivyo inaonesha jinsi gani Serikali inataka uvunaji wa rasilimali za uvuvi ufanyike na sekta ya uvuvi iweze kusaidia maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini. Kutokana na hali hiyo, mfumo wa mgawanyo na utumiaji wa rasilimali za uvuvi unajumuisha matakwa ya wananchi na serikali ambayo wakati mwengine ni mazuri na pia yanaweza kuleta migongano baina ya pande mbili hizo.

Vile vile, asili ya ushiriki wa dola katika usimamizi wa sekta ya uvuvi ni kuhakikisha kuwa uchumi unaimarika na jamii inanufaika kutokana na uvuvi na shughuli zinazohusiana na uvuvi. Aidha, ushiriki wa dola unahakikisha kwamba kila mtu ananufaika na uvuvi, pia uwezo wa uzalishaji upya wa rasilimali za uvuvi unalindwa ikiwemo mazingira ambayo husaidia uzalishaji huo.

Kwa kumalizia, na kwa muktadha wa Programu ya SmartFish, utawala bora katika uvuvi ni hali ambayo Dola inalazimika kuanzisha mfumo bora wa uongozi utakaojumuisha mhimili wa utawala endelevu na wenye kufuata misingi mengine ya utawala bora inayohusiana na utoaji wa huduma kwa jamii, kama vile uwazi, ushirikishwaji (ikiwemo usimamizi wa pamoja), ufanisi (thamani inayolingana na gharama) n.k.

Mhimili wa Utawala unaweza kufasiliwa kama jumla ya sera, taasisi, sheria, kanuni na huduma ambazo huathiri utumiaji, uongezekaji wa thamani na usimamizi wa uvuvi. Ili kuwa endelevu, mhimili wa utawala unapaswa kuzingatia mahitaji na sifa mahsusi za usimamizi wa rasilimali za uvuvi, makubaliano ya kimataifa na wajubu wa nchi kuhusiana na uvuvi unaozingatia uhifadhi wa mazingira na kulinda maliasiliza bahari. Mhimili pia unapaswa kuakisi malengo ya taifa na malengo yaliyopangiwa kufikiwa na sekta ya uvuvi.

2.2 KAZI NA NAFASI YA MKAKATI WA UTAWALA WA UVUVI KATIKA UTAWALA NA USIMAMIZI WA UVUVI

Mchakato wa kuandaa Mkakati kwa ajili ya kuimarisha Uongozi na Usimamizi wa Uvuvi Zanzibar umetokana na hamu ya kuwa na mtazamo mpya wa namna ya kutawala shughuli za uvuvi kinyuma na vile sekta hiii mekuwa ikisimamiwa hadi sasa. Aidha, uandaaji wa Mkakati huu unasaidia kufahamu namna gani sekta ya uvuvi inaendeshwa kwa sasa na mabadiliko gani yanahitajika katika utawala wa uvuvi ili kuweza kuimarisha sekta hii zaidi. Mchakato huu pia umefanyika huku ikifahamika kwamba Mkakati wa Utawala wa Uvuvi unalazimika kuifanya sekta ya uvuvi kuwa ni sekta itakayochangia kwa kiasi kikubwa zaidi katika maendeleo ya kiuchumi na kisiasa ya Zanzibar na wakati huo huo ikilinda ubora wa mfumo wa mazingira ya bahari.

Kwa hiyo, Mkakati wa Utawala wa Uvuvi, kwanza, hauna budi kutizamwa kama waraka wenye lengo la kutoa mwongozi wa kisera wa kuimarisha mfumo wa utawala wa uvuvi Zanzibar kwa muda usiozidi miaka mitano (5). Changamoto zilizopo ni pamoja na uimarishaji wa mhimili wote wa utawala (ambao hujumuisha utungaji wa sheria, kanuni, nyaraka za mipango, taasisi na huduma za usimamizi) pamoja na kuhimiza utekelezaji wa misingi ya utawala bora kwa ajiliya kujenga Dola Bora, huku mkazo ukiwekwa katika kupatikana kwa thamani halisi kwa mujibu wa juhudi zilizofanyika katika usimamizi wa uvuvi. Thamani na juhudi hizi zitapimwa kulingana bajeti na nguvu kazi iliyotumika.

Lengo la Mkakati wa Utawala wa Uvuvi ni kufikia malengo ya jumla yaliyowekewa sekta ya uvuvi kama

yalivyotajwa katika Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar wa 2020 (Vision 2020) na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar Sehemu ya Pili (MKUZA II). Mkakati unaweza kuchukuliwa kama waraka wa sera ya sekta ya uvuvi wenye kuelekeza namna gani sekta hii isimamiwe ili kufikiwa kwa malengo yaliyowekwa.

Uzoefu unaonesha kwamba utawala bora katika sekta ya uvuvi unapaswa kujumuisha wadau wote wa sekta hiyo, hasa Viongozi wa Uvuvi, wavuvi na wahusika wengine. Pia unapaswa kuzileta pamoja taasisi za serikali na binafsi zinazoshughulika moja kwa moja au kwa njia nyegine yoyote na usimamizi wa sekta hiyo.Miongoni mwa taasisi na asasi hizo ni ni taasisi za kielimu za utafiti, Jeshi la wanamaji, Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar, serikali za mitaa, kamisheni ya utalii, Wizara inayoshughulikia Mazingira, Wizara ya Elimu, Mashirika Yasiyo yaKiserikali (NGOs), n.k. Kutokana na sababu hizi, Mkakati wa Utawala wa Uvuvi unapaswa kuakisi mtazamo wa pamoja utakaotokana na kujengeka kwa makubaliano. Aidha, utekelezaji wa Mkakati huu utakukuwa ni jukumu la taasisi mbali mbali huku Uongozi wa Uvuvi ukiwa na kazi ya kuongoza uhamasihaji katika mchakato huo.

Kutokana na muktadha wa maelezo ya hapo juu, Mkakati wa Utawala wa Uvuvi utakuwa kama waraka wa kurejelea katika kusaidia mipango ya baadaye ya Uongozi wa Uvuvi. Zaidi ya hayo, Mkakati huu usaidie katika kuipitia upya Sera ya Uvuvi ya mwaka 2000.Huu ni waraka wa mipango wenye mambo mengi muhimu yatakayosaidia kutoa mwelekeowa kazi za vitengo mbali mbali vya Utawala wa Uvuvi. Hata hivyo, muda wa Mkakati huu usizidi miaka minne (4) au mitano (5). Sera ya Uvuvi iliyofanyiwa marekebisho (pamoja na sheria za uvuvi zilizotungwa) zinapaswa kuzingatiwa kama vyombo muhimu vya kusaidia utekelezaji wa Mkakati huu. Sera ya Uvuvi pia inatarajiwa kujumuisha kazi zenye lengo la kusaidia kuleta juhudi, ushirikiano na utendaji wa pamoja miongoni mwa taasisi za serikali na binafsi ilikupatikana kwa huduma za usimamizi ambazo ni muhimu kwa mafanikio ya Mkakati huu.

Mwisho, ni muhimu kusisitiza kwamba suala la kuimarisha utawala wa uvuvi ni la muda mrefu na lenye kupita hatua kwa hatua zinazoweza kujirudiarudia. Hivyo, linahitaja kuwepo kwa mwongozo utakaoonesha kazi zitakazopewa kipaumbele na mipago yake. Muda unaopendekezwa kwa Mkakati wa Utawala wa Uvuvi Zanzibar ni miaka saba (7) (yaani kuanzia 2014 – 2020) ili kwenda sambamba na Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar wa 2020 (Vision 2020). Kazi zilizowekwa katika mwongozo ni zile za muda mfupi hadi muda wa kati (ambazo ni za kati ya mwaka 1 hadi miaka 3) na zile za muda wa kati hadi muda mrefu (miaka 4 hadi 7). Utaratibu huu umewekwa ili kurahisisha utekelezaji.

2.3 MAMBO MUHIMU YA KISEKTA YATAKAYOZINGATIWA KATIKA MKAKATI WA UTAWALA WA UVUVI.

Kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar wa 2020 (Vision 2020) sekta ya uvuvi ni miongoni mwa sekta za mkakati wa kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii Zanzibar. Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar wa 2020 (Vision 2020) pia unaiunganisha sekta ya uvuvi na sekta ya utalii kwa kutilia mkazo umuhimu wa kuimarisha usimamizi wa rasilimali za pwani na baharini kwa lengo la kuleta maendeleo endelevu ya uvuvi huku zikilinda utajiri wa mazingira..

Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar wa 2020 (Vision 2020) na MKUZA II zimeiweka sekta ya uvuvi katika kundi ambalo lengo lake la msingi ni kushughulikia changamoto ya ukuaji kwa Zanzibar. Kundi hili linakusudiwa kukuleta matokeo makubwa ya “kufikia maendeleo ya uchumi endelevu kwa wote” na malengo manne kama yafuatayo:

(i) kutengeza mazingira ya ukuaji wa uchumi
(ii) kuimarisha mpango mpana endelevu wa maendeleo ya uchumi kwa wote
(iii) kupunguza umasikini wa kipato na kufikia lengo la jumla la usalama wa chakula
(iv) Kutengeneza sekta binafsi yenye ufanisi kwa ajili ya kuleta maendeleo ya kiuchumi

MKUZA II pia inatilia mkazo kwamba shughuli nyingi za uvuvi zinafanywa kwenye maji madogo, ambako hakuna uhakika na rasilimali za uvuvi zimeshatumika kwa kiasi kikubwa. Kwa upande mwengine kuna fursa kubwa wa maendeleo ya uvuvi mikondoni ambako rasilimali za uvuvi zimetumika kiasi au bado hazijatumika ipasavyo.

Kwa mujibu wa takwimu rasmi, uvuvi wa jumla katika bahari ya Zanzibar, ambao unajumuisha Bahari ya Zanzibar pamoja na eneo la ndani la bahari, umeongezeka kwa kiwango kikubwa katika miaka 10 iliyopita. Hii inaweza kuchukulia kama dalili ya jitihada za wavuvi na kwa kiasi fulani mafanikio ya sera za serikali katika sekta ya uvuvi. Sehemu ifuatayo itaonesha kwa upana zaidi hali ilivyo sasa kuhusu rasilimali za uvuvi pamoja na hatua ambayo sekta ya uvuvi imepiga kwa mujibu wa Vision 2020 na MKUZA II.

2.3.1 HATUA ILIYOPIGWA NA SEKTA YA UVUVI KWA MUJIBU WA MALENGO YA VISION 2020 NA MKUZA II

Uvuvi Endelevu wa Maji Madogo

Katika maeneo ya karibu na pwani, hasa katika maeneo yenye miamba, kumekuwa na hali ya upungufu wa uzaliwaji wa samaki na ukamataji wa samaki kwa wavuvi wadogo wadogo. Hii imechangiwa kwa kiasi kikubwa na sababu mbali mbali kama kuelemewa kwa sekta ya uvuvi, kufanyika sana kwa uvuvi wa karibu na pwani na uvuvi wa maji madogo unaofanyika katika maeneo ya mfumo wa mazingira ya miamba kunakosababishwa na kuwepo kwa teknolojia duni za uvuvi, na udhibiti mbaya wa shughuli za uvuvi unaosababishwa na mapungufu yaliyopo katika mfumo wa utawala na usimamizi wa sekta hiyo.

Kuelemewa kwa sekta ya uvuvi wa karibu na pwani na maji madogo kunaonekana kwa kuangalia ongezeko la uwezo wa kuvua linalosababishwa na kuongezeka kwa vyombo vya uvuvi, matumizi ya mashine, vifaa vinavyosaidia kuvua kwa ufanisi zaidi nyavu za mtando, nyavu kukokota na nyavu za duara. Ongezeko hilo pia limesababishwa kuimarika kwa uvumbuzi wa kiteknolojia (kama vile kuongezeka kidogo kwa urefu wa vyombo vya uvuvi) pamoja na kuvua katika eneo kubwa zaidi.

Sababu kuu nyengine za kuelemewa kwa sekta ya uvuvi wa karibu na pwani na maji madogo ni uhuru wa kuvua rasilimali za bahari zilizopo, uwezo mdogo wa wavuvi kuvua mikondoni, kupanda kwa kiasi kikubwa kwa bei ya samaki (ambako kunawapa moyo wavuvi kuendelea kuvua pamoja na upatikanaji mdogo wa samaki), na uwezo mdogo wa jamii za wavuvi wa kujitafutia shughuli nyengine za kujiongezea kipato.

Zaidi ya hayo, uvuvi hausimamiwi ipasavyo jambo ambalo linawafanya wavuvi wasifuate taratibu chache zilizopo zenye lengo la kudhibiti rasilimali za uvuvi na mazingira ya pwani, ikiwemo maeneo ya bahari yanayohifadhiwa.

Kwa hiyo, pamoja na kutokuwepo kwa ushahidi wa kisayansi, uvuvi wa karibu na pwani na maji madogo si wa uhakika kwa sababu kuna uwezekano wa kumalizika au kubakia kidogo kwa rasilimali za uvuvi (katika kiwango cha juu vinavyoweza kuzifanya rasilimali hizo kuwa endelevu, jambo ambalo linaonesha wazi kwa nini kuna upatikanaji mdogo sana wa rasilimali hizo kinyume na jitihada zinazofanywa na wavuvi) na kwa wavuvi kutokufuata kanuni za uvuvi. Aidha, uvuvi wa maji madogo hanuna uhakika kutokana na idadi kubwa ya wavuvi wanaovua katika sehemu hizo.

Maendeleo ya Uvuvi Mdogo Mikondoni

Katika miaka ya karibuni iliyopita na mpaka sasa, hatua mbali mbali zimechukuliwa kwa lengo la kusaidia uvuvi mdogo kufanyika mikondoni. Mkazo umewekwa katika kuendeleza uvuvi wa kutumia Maumbo Yanayowavutia Samaki (FAD) na kulenga kuvua samaki wakubwa na wa saizi ya kati wanaopatikana

zaidi katika bahari kuu ambao hawajavuliwa kwa kiwango kikubwa. Hata hivyo, maeneo bahari kuu na mengine ya bahari ya taifa bado hayajatumika ipasavyo kwa shughuli za uvuvi. Hali hii inatokana na kushindwa kwa sera za serikali za kutengeneza mazingira bora ambao yangeweza kuleta pamoja teknolojia, rasilimali watu, fedha, taasisi zinazojihusisha na uvuvi na masoko katika maendeleo ya uvuvi. Kwa upande mwengine, uzoefu uliopatikana kutokana na hatua zilizochukuliwa huko nyuma unaweza kusaidia uanzishaji wa mikakati bora zaidi kwa ajili ya mipango ya baadaye.

Maendeleo ya Kilimo cha Baharini

Kilimo cha mwani kimekuwa mara dufu katika muongo uliopita na kwa sasa ni mapato na maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa jamii zinazoishi pembezoni mwa bahari. Hata hivyo, zao hilo linakabiliwa na tatizo la ongezeko la thamani (bei ndogo ya kuuzia) hivyo kuathiri upatikanaji wa tija katika shughuli zinazoambatana za kilimo chake na matokeo yake kushindwa kuchangia ipasavyo kuondoa umasikini kwa jamii za pwani, hasa wanawake. Pia kilimo cha mwani kinasadikiwa kuchangia mmong'onyoko wa fukwe kwani mwani huchukuwa nafasi ya majani ya bahari yanayoota kwenye ardhi ndani ya bahari ambayo ni aula zaidi kuzuia mmong'onyoko unaosababishwa na maji. Shughuli nyengine za kilimo cha baharini zinazoibuka na zenye mwelekeo wa kuleta tija ni ufugaji wa samaki, lulu, kamba, na kaa. Hata hivyo, shughuli hizi bado zipo katika kiwango cha chini.

Kuna changamoto kubwa za kiuchumi, kijamii na kimazingira katika kilimo cha baharini Zanzibar. Wakati huo huo, kama ilivyo kwa nchi nyingi duniani, kilimo cha baharini kinawahusisha zaidi wajasiriamali na wanawake. Hii ni kwa sababu kilimo hiki hakichukuliwi na wavuvi kama shughuli mbadala ya kiuchumi inayoweza kupunguza kiwango kikubwa cha uvuvi wa maji madogo.

Kupunguza Umasikini katika Jamii za Wavuvi

Tatizo jengine la utekelezaji mbaya wa shughuli za uvuvi wa maji madogo na ugumu wa kuendeleza uvuvi wa bahari kuu ni uwezekano wa kupatikana tija ndogo au kutopatikana kabisa kwa tija (au utajiri) katika shughuli za uvuvi siku hizi huku tija inayopatikana sasa ikupungua kwa kasi kubwa. Kwa hiyo, inaaminika kwamba umasikini katika jamii za wavuvi unaongezeka sana kutokana na kipato kidogo au kutokua kwa kipato cha jumla miongoni mwa wavuvi ambao wanaongezeka kwa kasi. Katika baadhi ya sehemu hali hii imesababisha migongano miongoni mwa wavuvi inayotokana na kugombania maeneo yenye samaki.

Kuongezeka kwa Mchango wa Sekta ya Uvuvi katika Usalama wa Chakula

Wastani wa matumizi ya samaki kwa Zanzibar yameendelea kuwa makubwa ukilinganisha na nchi nyengine zilizopo katika ukanda huu. Hii imetokana na ongezeko la samaki wanaozalishwa nchini. Hata hivyo, viwango vya ubora wa aina mbali mbali wa samaki bado havijafikiwa. Aidha, samaki wenye thamani kubwa na ubora ambao mara nyingi hupatikana katika bahari kuu na chini ya bahari wanatumiwa zaidi na watalii, hivyo kuwanyima fursa walaji wenyeji. Hii inaonesha haja iliyopo ya kukuza uvuvi wa kutumia Maumbo Yanayowavutia Samaki (FAD) kwa lengo la kukamata samaki kama jodari na wengine wa aina hiyo ambao watawatosheleza mahitaji ya utalii ya kuwa na samaki wa ubora wa juu na wakati huo huo watosheleza kwa matumizi wa walaji wazawa.

Uwiano baina ya Maendeleo ya Uvuvi na Sekta ya Utalii

Uchumi wa Zanzibar unategemea sana kilimo (ikiwemo uvuvi) na sekta ya utalii ambayo inachangia thuluthi moja ya Pato la Ndani. Utalii ni muhimu sana katika muundo wa sasa wa uchumi wa Zanzibar katika muktadha wa kwamba biashara hii inategemea sana utajiri wa mfumo wa mazingira ya miamba na uzuri wa kimaumbile wa mazingira. Katika kushughulikia kuanzisha mpango mzuri wa kuendeleza utalii wakati huo huo mfumo wa mazingira ya pwani yakilindwa, Serikali ya Zanzibar, ikishirikiana na washirika mbali mbali, imesaidia katika utayarishaji wa mtandao wa kulinda maeneo muhimu ya bahari (Uhifadhi wa Maeneo ya Bahari – Maeneo ya Hifadhi ya Bahari). Sera hii imeleta matokeo

mazuri katika kulinda utajiri wa mifumo muhimu ya mazingira. Hata hivyo, utekelezaji wa Uhifadhi wa Maeneo ya Bahari, hasa katika shughuli za ulinzi umekuwa kwa kiasi kikubwa ukitegemea ufadhili kutoka miradi ya nje ya nchi na ni vigumu kuendelea kwa muda mrefu bila ya kuwepo kwa mabadiliko ya kitaasisi na kisheria yatakayosaidia kuimarisha utawala wa Maeneo ya Hifadhi ya Bahari

Hali mbaya ya sasa ya usimamizi wa uvuvi wa maji madogo Zanzibar, ikiwemo katika Maeneo ya Hifadhi ya Bahari, inaweza, pole pole, kuleta athari mbaya kwa mfumo wa mazingira ya bahari, ikiwemo mimea na wanyama, na hatimaye uwezekano wa kuleta madhara katika sekta ya utalii

Suluhisho la awali ni kwamba pamoja na ongezeko la uzalishaji wa samaki, hali ya sasa ya rasilimali za uvuvi katika maeneo ya miamba na utekelezaji wa sekta ya uvuvi haviridhishi katika kufikia malengo ya jumla yaliyotajwa katika Vision 2020 na MKUZA II.

Pia kuna matatizo uchangamani na ugumu yanayokabili usimamizi wa uvuvi wa maji madogo, ambayo ni pamoja na kuwa ni uvuvi mdogo, unaohitaji vifaa vingi na kuvua samaki wa aina. Hali hii pia imetokana na kukosekana kwa uendelevu na mfungamano kati ya vipengele mbalimbali vya mhimili wa utawala wa uvuvi na kutotekelezwa ipaswavyo kwa misingi wa utawala bora katika utekelezaji wa sekta ya uvuvi.

2.3.2 UPUNGUFU NA UDHAIFU MKUU KATIKA MFUMO WA SASA WA UTAWALA

Upungufu na udhaifu uliopo katika mfumo wa sasa wa Utawala wa Uvuvi unaweza kuelezwa kwa ufupi kama ifuatavyo:

Sera ya Uvuvi ya Zanzibar Yenye Kasoro na Iliyopitwa na Wakati. Hali hii inaikosesha sekta ya uvuvi waraka ambao ungeainisha wazi mwelekeo na mkakati wenye vipaumbele vinavyohitajika kutekelezwa na ambayo ingekuwa ni mwongozo wa kupangilia shughuli za Uongozi wa Uvuvi. Waraka huo ungeweza kusaidia kuimarisha ushiriki mzuri wa wadau kutoka serikalini na sekta binafsi wanaoshughulikia masuala ya maendeleo na usimamizi wa uvuvi. Sera hiyo kwa sasa ipo kama mpango kazi wa Uongozi wa Uvuvi, ikionesha zaidi muundo wa kiutawala na malengo ya Idara inayosimamia Uvivi katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi (WMU) badala ya kuonesha vipaumbele vinavyopaswa kuandaliwa ili kuweka mazingira mazuri ya kuwepo uvuvi unaojalimazingira kwa mujibu wa Mwelekeo wa 2020 na MKUZA II.

Udhaifu wa Mhimili wa Sheria na Kanuni za Uvuvi. Kwa ujumla mambo haya hayajakamilika (Kanuni zinazoipa nguvu Sera ya Uvuvi ya mwaka 2000 bado hazijapitishwa). Hali hii inaleta mkanganyiko katika kanuni zilizopo sasa na kupelekea kuwepo ugumu wa utekelezaji wa vipengele muhimu vya sera kama vile utendaji kazi wa Maeneo ya Hifadhi ya Bahari (MCAs) na utoaji wa huduma muhimu za Usimamizi kama vile Ufatiliaji, Udhibiti na Ulinzi (MCS). Pia sheria iliyopo inampaWaziri nguvu kubwa ya uamuzi nje ya sheria na wakati huo huo haishajiishi matumizi ya misingi mingine muhimu ya utawala bora ikiwemo ushirikishwaji na uwazi.

Matatizo yaliyonazo taasisi za Serikali katika utoaji wa kuridhisha wa huduma muhimu za usimamizi wa Uvuvi. Huduma hizi ni kama zifuatazo: Nafasi za kisheria za wahusika wa kiuchumi wanaojishughulisha na uvuvi na kazi nyengine zinazohusiana na uvuvi (yaani wavuvi, wasindikaji wa samaki, wachuuzi), mafunzo na uenezi, utafiti, ufuatiliaji wa uvuvi, udhibiti na ulinzi (MCS), na usimamizi wa utii wa sheria. Sababu zinazopelekea kutokea kwa hali hii ni pamoja na udhaifu wa kitaasisi na kiubinadamu, matatizo ya kifedha na kimipango inayoukabili Uongozi wa Uvuvi, kwa Makao makuu na katika maeneo ambayo shughuli za uvuvi hufanyika, kwa visiwa vyote vya Unguja na Pemba.

Kutotiliwa maanani kwa kiasi kikubwa mashauriano na wadau wa uvuvi wakati wa kufanya maamuzi na kuandaa taratibu za mashirikiano katika ya serikali na sekta binafsi, hasa nje ya

Maeneo ya Hifadhi ya Bahari (MCAs), kwa lengo la kutoa huduma muhumu za usimamizi wa uvuvi.

Udhaifu katika utaratibu wa mashirikiano na Tanzania Bara katika kushughulikia masuala yanayozigusa pande zote mbili kwa pamoja kama vile kusaidia usimamizi wa pamoja wa rasilimali za pamoja zinazopatikana katika bahari kuu.

Katika muktadha huu, kazi za serikali katika sekta ya uvuvi ni pamoja na kushughulikia kazi za kila siku za ukusanyaji wa takwimu, kuzuia hatari kubwa zinazohusiana na Uvuvi Haramu na Usiofuata kanuni, kusuluhisha migogoro ya ndani na kutafuta fedha zaidi kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa Uhifadhi wa Maeneo ya Bahari (MCAs)

Uongozi wa uvuvi pia umefanya jitihada kubwa katika kusaidia jamii za wavuvi katika kuanzisha shughuli mbadala za kujipatia kipato ili kupunguza uvuvi mwingi unaoathiri miamba ya matumbawe. Shughuli hizo ni pamoja na kuimarisha kilimo cha baharini na uvuvi wa mbali na pwani kwenye bahari kuu. Mkazo pia umewekwa katika kuimarisha miradi ya kushughulikia samaki waliovuliwa ili kuinua kiwango cha ubora wa samaki kwa walaji na kupandisha bei ya samaki kwa mvuvi kwa ajili ya kufidia idadi ndogo ya samaki wanaopatikana.

Pia ni vyema itiliwe mkazo kwamba huduma za serikali katika sekta ya uvuvi zinategemea sana misaada kutoka nje ya nchi, jambo ambalo linaathiri ukuaji na maendeleo ya sekta hiyo. Kwa mfano, ulinzi katika Maeneo ya Hifadhi ya Bahari haujawa na ufanisi tokea kukamilika kwa Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na Pwani (MACEMP) uliokuwa ukifadhiliwa na Benki ya Dunia. Aidha, kutokana na kutokuwepo kwa Mwelekeo na Mkakati madhubuti, kazi zinazofanywa na serikali zimekuwa ni zile zinazohusiana na utekelezaji wa miradi/mipango maalumu isiyo na ushirikishwaji na ambayo haihusiani (kwa mfano kusaidia Kamati za Uvuvi za Vijiji, kufanya tafiti katika maeneo maalumu yaliyoteuliwa, kuingiza Maumbo Yanayowavutia Samaki (FAD), kuimarisha uwezo wa Ufuatiliaji, Udhibiti na Ulinzi (MCS) n.k.) hivyo, kwa jumla, kusababisha matokeo na ufanisi mdogo.

2.3.3 UBORA NA FURSA ZILIZOMO KWENYE MFUMO WA UTALAWA

Ubora na fursa zilizomo katika mfumo wa sasa wa uongozi wa uvuvi ni kama ufuatao:

Kuwepo kwa utaratibu wa mashirikiano kati ya Uongozi wa Uvuvi na Tasisi nyengine za serikali, hususan katika masuala ya Ufuatiliaji, Udhibiti na Ulinzi (MCS) na usimamizi wa utii wa sheria, vile vile kuunganisha Mpango Shirikishi wa Usimamizi wa Ukanda wa Pwani (ICZM)

Kuwepo kwa Mtandao wa Maeneo ya Hifadhi ya Bahari (MCAs) ambayo yanalindwa na Amri na ambayo kazi zake zinaweza kuimarishwa zaidi iwapo mswada wa kanuni za Kitengo cha Hifadhi ya Bahari (MCU) zitaidhinishwa. Uzoefu unaonesha kwamba Maeneo ya Hifadhi ya Bahari (MCAs) ni nyenzo za kutosha za kisera za kuimarisha usimamizi na utawala wa uvuvi katika maeneo ya hifadhi yaliyotangazwa, hasa kanuni maalumu zinapotumika (kama maeneo yasiyoruhusiwa kuvua, kuzuia matumizi ya baadhi ya zana za uvuvi, kupiga marufuku kambi za wavuvi wageni).Nyenzo nyengine ni mifuko ya maendeleo ya jamii, kuandaa mikutano itakayosaidia majadiliano kati ya Uongozi wa Uvuvi na wadau wengine binafsi na kutoka serikalini na kutoa fursa kwa jamii za wavuvi kuziimarisha sheria ndogo maalumu.

Kuwepo kwa Mtandao wa Kamati za Uvuvi za Vijiji (VFCs) hususa katika Maeneo ya Hifadhi ya Bahari (MCAs), ambazo zinaweza kuwa msingi wa kuundia mikakati ya ushirikishwaji zaidi wa wadau katika mipango na usimamizi. Ni vyema ifahamike kwamba kuna mfumo imara wa uvuvi wa asili katika jamii za pwani, jambo ambalo linaweza kuchukuliwa kama rasilimali kama inavyoonekana katika mpango wa usimamizi wa pamoja ulioanzishwa na Uongozi wa Uvuvi

Mipango inayoendelea yenye lengo la kupanua mtandao wa Maeneo ya Hifadhi ya Bahari Zanzibar ambayo inaashiria utayari wa kisiasa katika kushughulikia uendelezaji wa uvuvi wa karibu na pwani wakati huo huo ukiendelea kuhifadhi mfumo wa mazingira ya pwani.

Miradi ya Maendeleo inayoendelea kutayarishwa ikiwemo mradi wa SWIOFish maalumu kwa Tanzania ambao unazingatia zaidi kuimarisha utawala na usimamizi wa Uvuvi bahari ya ndani na Bahari yote ya Zanzibar.

Kuwepo kwa Kitengo cha Utafiti katika Wizara Inayohusika na Uvuvi ambacho kina nafasi ya kufanya kazi muhimu ya kuimarisha mfumo wa utafiti wa uvuvi na ni vizuri kwamba Kitengo hicho kimewekwa katika Wizara inayoshughulikia Uvuvi kwani kitaweza kuunganisha tafiti na uundaji wa sera.

Kuwepo kwa Mfuko wa Maendeleo na Usimamizi wa Uvuvi ambao unaweza kuwa nyenzo muhimu ya kuchangia upatikanaji wa fedha kila zinapohitajika na hivyo kuendeleza kazi za serkali za kuongoza na kusimamia uvuvi Zanzibar, hasa katika Maeneo ya Hifadhi ya Bahari (MCAs).

3. MALENGO NA MISINGI ELEKEZI YA MKAKATI WA UTAWALA WA UVUVI

3.1 MALENGO YA MKAKATI WA UTAWALA WA UVUVI

Malengo ya Mkakati wa Utawala wa Uvuvi, ambayo utekelezaji wake inajumuisha Taasisi za serikali na binafsi ambazo zinajishughulisha na masuala ya uvuvi moja kwa moja au kwa njia nyengine yoyote, ikiwemo Uongozi wa Uvuvi, yanakwenda sambamba na malengo ya Mwelekeo wa 2020 na MKUZA II.

Malengo ya Mkakati wa Utawala wa Uvuvi yatakuwa ni:

Kuhakikisha kunakuwa na rasilimali endelevu za uvuvi na kusaidia kulinda wanyama na mimea katika mfumo wa mazingira ya miamba, jambo ambalo pia litachangia maendeleo endelevu ya utalii na shughuli nyengine zinazohusiana na utalii.

Kuongeza ufanisi wa kijamii na kiuchumi katika sekta ya Uvuvi kwa kuimarisha usimamizi wa uvuvi wa karibu na pwani, kuweka mazingira mazuri ya kuendeleza uvuvi mdogo kwa kuweka lengo la kuvua aina za samaki na rasilimali nyengine za bahari ambazo hawavuliwi vya kutosha katika bahari kuu, na kutilia mkazo maendeleo ya kilimo cha baharini.

Kuongeza usambazaji wa samaki na kuinua ubora wa samaki na mazao yanayotokana na samaki kwa mujibu wa matakwa ya usalama wa chakula kwa wakazi wa Zanzibar, pia kufikia viwango vya kimataifa.

3.2 MISINGI ELEKEZI MIKUU

3.2.1 USIMAMIZI WA UVUVI WA KARIBU NA PWANI

Itakuwa ni jambo gumu sana kubadilisha tabia iliyozoeleka ya uvuvi wa maeneo ya karibu na pwani kwa muda mfupi hadi muda wa kati kutokana na gharama kubwa kisiasa, kijamii na kitaasisi. Gharama hizi ni kwa ajili ya uchukuaji hatua madhubuti za kuzuia uvuvi wa aina hiyo. Aidha, itakuwa ni vigumu sana kuimarisha usimamizi wa uvuvi unaozingatia mapato makubwa kwa maeneo yote ya karibu na pwani kwa muda mfupi hadi wa kati. Uchangamani wa mambo yanayohusiana na uvuvi (kama vile vifaa

mbali mbali vya kuvulia na kuwepo kwa samaki wa aina tafauti), kutokuwepo kwa elimu ya kutosha ya sayansi, kuaminika sana kwa mfumo wa kuvua kwa uhuru bila vikwazo vyovyote, kupanda kwa bei ya samaki kunakotokana na kufidia upatikanaji mdogo wa samaki, utamaduni iliojengeka wa watu kujishughulisha sana na kazi ya uvuvi unaowafanya wavuvi kutotaka kuiacha kazi ya uvuvi na kuingilia kati kwa wanasiasa wenyeji katika masuala ya uvuvi ni miongoni mwa sababu kuu zinazoonesha kuwepo kwa gharama kubwa ya kubadilisha uvuvi wa karibu na pwani. Kwa hivyo, mchakato wa kuleta mabadiliko katika sekta ya uvuvi unapaswa kwenda kwa awamu na kutilia mkazo hatua za vipaumbele ili tija ipatikane kwa mujibu wa gharama zilizotumika. Hii pia ifanyike ili kulinda kupotea kwa akiba ya samaki na kuharibiwa kwa mfumo wa mazingira ya miamba.

Kwa maneno mengine, ni lazima ikubalike kwamba wavuvi wanaweza, kwa muda mdogo, kuvua kupita kiasi lakini katika namna ‘endelevu’ (yaani Zaidi ya Kiwango kinachoweza kuwafanya samaki waendelee kuzaliwa (MSY) lakini bila kumaliza kabisa akiba ya samaki). Hii itawezekana kwa kuwepo utekelezaji mzuri wa mipango ya kitaalamu ya usimamizi inayopewa kipaumbele na kuweka masharti ambayo yataruhusu kuwepo kwa kanuni zaidi kuhusu kiwango na uwezo utakaoruhusiwa kutumika katika kuvua. Pia, kufanya mabadiliko, pole pole, katika masuala ya usimamizi wa uvuvi wa bahari ya karibu na pwani.

Ili kutekeleza misingi hii elekezi kwa ajili ya usimamizi wa uvuvi wa bahari ya karibu na pwani, mambo yafuatayo yanapaswa kuzingatiwa:

Kuzuia pole pole uvuaji huru isiokuwa na vikwazo vyovyote na kushajiisha wavuvi na watu wengine wanaohusika na kazi za uvuvi kutumia utaalamu na kufuata taratibu.

Kuanzisha hatua kwa hatua mchakato wa kudhibiti kiwango cha uvuaji wa samaki katika maeneo ya karibu na pwani (Ndani na nje ya Maeneo ya Hifadhi ya bahari ili kuzuia kuhatarisha kutopatikana kwa mafanikio ya rasilimali za bahari zilizomo katika Maeneo ya Hifadhi ya Bahari – MCAs).

Kuelimisha dhana ya Kanuni ya Kipaumbele cha Kusimamia sheria ipasavyo (Priority Regulation for Strong Enforcement – PSE) ikiwemo maeneo yanayodhibitiwa kama vile Maeneo ya Hifadhi ya Bahari (MCAs).

Dhana ya PSE itajumuisha kutilia mkazo Ufuatiliaji, Udhibiti na Ulinzi (MCS) na kuongeza juhudi katika kusimamia kanuni zinazopea kipaumbele (kwa sababu za kibaiolojia, kijamii na au kiuchumi), hasa katika maeneo nyeti yaliyoteuliwa na ambayo ni rahisi kanuni hizo kutiiwa kwa asilimia 100. Hata hivyo, uzoefu unaonesha kwamba kwa kudhamiria utii wa kanuni wa asilimia 100 si jambo linaloweza kutekelezeka katika hali halisi katika mazingira ya siku hizo, jambo ambalo linaleta athari hasi kwa ufanisi wa jumla wa Ufuatiliaji, Udhibiti na Ulinzi (MCS) na pia kuathiri utii wa kanuni kwa hiari. Kwa hiyo, inashauriwa kwamba mkazo uwekwe katika orodha ya hatua za kipaumbele zenye lengo la kuridhiwa kwa asilimia 100 na nyengine zitekelezwe hatua kwa hatua wakati mfumo wote utakapofanikiwa. Mbinu ya PSE pia itaongeza viwango vya adhabu na vikwazo ikiwa kutakuwa na ukiukwaji wa sheria katika hatua hizo za kipaumbele ili kuongeza hofu ya uvunjaji sheria. Pia, kuongeza juhudi katika Ufuatiliaji, Udhibiti na Ulinzi (MCS), kufungua mashtaka na kupunguza uingiliaji kati ya siasa katika kanuni hizi za vipeumbele.

Kuongeza juhudi ili Maeneo ya Hifadhi ya Bahari (MCAs) yaendelee kufanya kazi kwa ufanisi, ikiwemo kuimarisha utawala wa maeneo hayo (usimamizi, ushirikishwaji wa wavuvi, kuziunganisha na usimamizi wa maeneo ya pwani, kuwepo kwa fedha n.k.). Kufanyakazi kwa maeneo ya Hifadhi ya Bahari ni vyema kuonekane kama hatua ya haraka na ya awali ya kuhakikisha kunakuwa na maendeleo endelevu ya uvuvi wa karibu na pwani. Aidha, ufanyaji kazi wa Maeneo ya Hifadhi ya Bahari ulinde wanyama na mimea vinavyopatikana katika maeneo ya mfumo wamazingira ya miamba ili kuwanufaisha wavuvi na watumiaji wengine, kama sekta ya utalii.

Kuimarisha juhudi za kushiriki utoaji wa elimu juu ya hatua zinazochukuliwa katika Mpango Shirikishi

wa Usimamizi wa Ukanda wa Pwani (ICZM) na kuimarisha mfumo wa taifa wa kuhifadhi na kupiga vita uchafuzi wa mazingira ya bahari kwa madhumuni ya kuendeleza mfumo ya mazingira miamba ya matumbawe.

Kuimarisha uhamishaji wa uwezo na juhudi za uvuvi kutoka maji madogo kwenda bahari kuu maeneo ya mbali na pwani, huku maendeleo ya uvuvi wa kutumia Maumbo Yanayowavutia Samaki (FAD) ukiimarishwa (Angalia chini)

Kuanzisha Mipango ya Usimamizi wa Uvuvi (Fisheries Management Plans – FMP) katika maeneo maalumu ya uvuvi yatakayoteuliwa kulingana na mfanano wake kibaiolojia, kijiografia, kijamii na/ au kiuchumi, na pia kuangalia ni Mipango gani ya Usimamizi wa Uvuvi inyoweza kutekelezwa. Kwa mfano, vitengo vya usimamizi wa uvuvi vinavyofaa ambavyo Mipango ya Usimamizi wa Uvuvi inaweza kuvianzisha, katika muktadha wa sasa wa Uvuvi wa Zanzibar, ni pamoja pweza, kaa, majongoo ya pwani na samaki wadogo (kwa kitengo cha mwisho uwepo ushirikiano na Tanzania Bara).

Kuziwezesha jamii za wavuvi kupata programu za elimu kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kutatua migogoro kwa ufanisi na kujitafutia shughuli nyengine za kipato nje ya sekta ya uvuvi.

Kuimarisha mbinu za jamii za wavuvi za kwenda sambamba na mabadiliko ya tabia nchi.

3.2.2 MAENDELEO YA UVUVI MBALI NA FUKWE KWENYE BAHARI KUU

Matumizi ya Maumbo Yanayowavutia Samaki (FAD) yanatoa nafasi ya kuongeza upatikanaji wa samaki katika maeneo ya bahari milki ya Zanzibar na maeneo ya bahari ya ndani. Ili kuwavutia kwa muda samaki wanaopatikana katika bahari kuu, vifaa hivi (vyenye maumbo yaliyounganishwa na maboya) huwasaidia wavuvi wadogo kupata samaki ambao awali ilikuwa ni vigumu kwao kuweza kuwafikia (kwa sababu hawavui zaidi ya sehemu zenye miamba ya matumbawe na wanatumia mashua zisizokwenda kasi na kufanya wasiweze kurambaza katika makundi ya samaki). Vile vile matumizi ya Maumbo Yanayowavutia Samaki yanaweza kusababisha kubadilisha aina ya uvuvi kutoka ule wa karibu na pwani usio na tija kubwa kwenda uvuvi mbali na pwani kwenye bahari kuu katika maeneo maalumu ambako samaki aina ya jodari na wengine wa aina hiyo hupatikana. Hii itapunguza kuzidiwa nguvu kwa uvuvi wa karibu na pwani. Pia ni vyema kusisitizwa kwamba akiba kubwa ya samaki walio mbali na pwani katika bahari kuu bado hawajavuliwa ipasavyo, hivyo matumizi ya Maumbo Yanayowavutia Samaki (FAD) hautegemewi kuleta athari hasi kwa rasilimali za bahari, hasa ikizingatiwa kwamba samaki wachanga hawaruhusiwi kuvuliwa. Kwa hiyo, Maumbo Yanayowavutia Samaki (FAD) yanaweza kufanikisha kazi mbili, kwanza kama mfumo/mbinu yenye ufanisi katika uvuvi, ufanisi ambao utapelekea hali za kijamii na kiuchumi za wavuvi wadogo kuimarika na wakati huo huo sekta ya uvuvi kuchangia katika pato la ndani ya nchi (GDP) (ikiwemo kuondoa umasikini) na kuleta usalama wa chakula. Pili, FAD ni nyenzo itakayosaidia usimamizi wa uvuvi wa karibu na pwani. Pia ikumbukwe kwamba Maumbo Yanayowavutia Samaki (FAD) yanasaidia kuendeleza michezo ya uvuvi.

Hatua mbali mbali za kuendeleza uvuvi wa Maumbo Yanayowavutia Samaki zimechukuliwa katika eneo la Kusini Magharibi ya Bahari ya Hindi, ikiwemo Zanzibar, katika miongo miwili iliyopita. Hatua hizi zilichukuliwa kupitia ufadhili wa miradi. Aidha, ufanisi wa uvuvi wa Maumbo Yanayowavutia Samaki umethibitishwa. Hata hivyo, matunda ya uvuvi wa Maumbo Yanayowavutia Samaki katika kutatua changamoto za kiuchumi na kiusimamizi yamekuwa na tafauti kubwa na miradi mingi imeshindwa kuendelea baada ya kukalimilika muda wa mradi husika. Pamoja na hali hiyo, hatua zote hizo zimetoa mafunzo muhimu sana, hasa katika masuala ya utawala. Mafunzo yaliyopatikana katika hatua hizo yamezingatiwa katika uandaaji wa Mkakati huu. Miongoni mwa mafunzo yaliyopatikana kutokana na uzoefu wa awali ni kwamba mipango ya kuendeleza uvuvi wa Maumbo Yanayowavutia Samaki inapaswa kuingizwa katika mkabala wa kuunganisha maendeleo na usimamizi, huku vipengele vya teknolojia, jamii, uchumina biashara vikiizingatiwa. Kwa maneno mengine, mkakabala utakaozingatia matumizi ya FAD peke yake una uwezekano wa kutoleta matokeo ya kuridhisha.

Misingi mahsusi elekezi inayopatikana kutokana na uzoefu na mafunzo yaliyopatikana awali ni haya yanayowasilishwa hapo chini. Mengi yao yanatokana na utafiti uliofanyika hivi karibuni kwa udhamini wa West Indian Ocean Fisheries Project (SWIOFP)[2]

Mafanikio ya matumizi ya FAD katika kuongeza idadi ya samaki wanaopatikana na uteuzi wa aina ya samaki wa kuvua kwa kiasi kikubwa kunategemea teknolojia inayotumika. Kwa hivyo, kuna haja ya kuwashajiisha wataalamu wa fani tafauti kushiriki hatua mbali mbali za mchakato wa kuendeleza uvuvi (kwa mfano, wataalamu wasiopatikana Tanzania, hasa katika teknolojia ya uvuvi). Teknolojia inakusudiwa kuyafanya matumizi ya FAD yaendane na mazingira ya eneo litakalotumika kwa uvuvi (kwa mujibu wa aina ya bahari na hali za kijamii na kiuchumi). Mambo mengine ya kuzingatia ni aina Maumbo Yanayowavutia Samaki zitakazotumika, vyombo na mbinu za uvuvi zinazopaswa kutiliwa mkazo, mafunzo ya uvuvi na usalama baharini kwa wavuvi n.k. Utoaji wa fursa za mikopo kwa ajili ya kununua vyombo na vifaa maalumu vya uvuvi ni miongoni mwa masharti ya kufanikisha mpango huu.

Mafanikio ya kutumia FAD pia yanategemea kuwepo kwa soko la kutosha la samaki. Mahitaji ya samaki wakubwa kama jodari na wengine wa aina hiyo yanaweza kuwa makubwa hasa kwa msaada wa sekta ya utalii. Hata hivyo, wavuvi wanaweza kukidhi vyema masoko ya samaki iwapo hakutakuwa na matatizo ya uhifadhi (katika mafriji na barafu) na usafirishaji wa samaki mara wanaporudi kuvua. Hii inaonesha kwamba hatua zozote za kuendeleza uvuvi wa FAD ni lazima zishughulikia maendeleo ya miundombinu na nyenzo nyengine muhimu katika bandari za uvuvi maalumu zitakazoteuliwa. Pia, nyenzo hizi zizingatie uchambuzi wa mtiririko wa thamani.

Mafanikio ya FAD pia yatategemea utekelezaji wa mpango maalumu wa matumizi ya Maumbo Yanayowavutia Samaki (FAD) wenye lengo la kuweko utaratibu maalumu kwa kutumia vifaa hivyo. Mpango huo uanzishe utaratibu wa upatikanaji na mwongozo wa matumizi ya FAD. Utaratibu huo pamoja na mambo mengine utashughulikia leseni na kanuni (zikiwemo aina za vifaa vinavyofaa kutumika kuvulia, aina ya samaki wanaoweza kuvuliwa, ukubwa wa samaki wanaoweza kuvuliwa, na misimu ya kuzuia uvuaji wa samaki). Mpango hup pia uzingatie Ufuatiliaji, Udhibiti na Ulinzi (MCS) na suala la usalama baharini.

Ushiriki wa wavuvi katika hatua mbali mbali za uandaaji wa programu ya uvuvi wa kutumia FAD ni muhimu sana kwa mafanikio ya programu hii. Umuhimu huo upo, kwanza, katika kuhakikisha kwamba kuna maendeleo na huduma za usimamizi za kutosha, na kupunguza hatari za migongani ndani ya jamii na kati ya jamii moja na nyengine.

Vile vile, maendeleo ya uvuvi wa Maumbo Yanayowavutia Samaki (FAD) unategemea mafanikio katika kuongezeka kwa upatikanaji wa samaki na mapato. Lakini pia, yanategemea kwa kiasi kikubwa kuwepo kwa mkakati wa matengenezo na ubadilishaji wa vifaa hivyo.

Kwa muktadha huo, suala la utaalamu linahitajika ili kupunguza gharama za matengenezo na ubadilishaji wa vifaa. Kwa mfano, Vifaa vya Kuvutia Samaki vitengenezwe katika hali ambayo vitaharibika katika sehemu ya juu pekee ikitokea hali mbaya ya hewa, kugongana, ajali wakati wa kurambaza, n.k. na pia kuweza kubadilishika ikibidi. Jambo muhimu la kuzingatia, hata hivyo, ni uhalali wa FAD. Katika suala hilo kuna hali mbili. Hali ya kwanza, ambayo imekuwa ikipendelewa zaidi katika eneo hili ni kwamba wajibu wa kufanya matengenezo na kubadilisha FAD uwe wa wavuvi wenyewe baada ya ufadhili wa mradi kumalizika. Katika muktadha wa uvuvi mdogo, hali haii haijaonesha mafanikio. Hali ya pili, ambayo inaweza kufanyiwa majaribio Zanzibar, ni kuyafanya Maumbo Yanayowavutia Samaki kuwa mali ya umma, na kwamba wajibu wa kufanya matengenezo na kuvibadilisha uwe kwa wakala maalumu atakayesaidiwa

2 Failler na wenzake (2011). Socio-economic assessment of Local FAD Fisheries in the South West Ocean. COFREPECHE.

kifedha (kwa mfano kwa kulipia gharama za haki ya kupatiwa Maumbo Yanayowavutia Samaki – FAD).

Mwisho kabisa, mafanikio ya Maumbo Yanayowavutia Samaki (FAD), kama msingi wa kuibuka kwa aina mpya ya uvuvi na kama nyenzo inayosaidia udhibiti wa uvuvi wa bahari ya karibu na pwani, yanahitaji ufuatiliaji wa karibu. Kazi za ufuatiliaji ni muhimu katika kukabiliana na matatizo yanayoweza kutokea katika sekta ya uvuvi au matokeo yasiyotarajiwa ambayo yatakuwa ni kinyume na malengo yaliyowekwa ya utekelezaji wa uvuvi wa FAD, pia kwenda sambamba na hatua zinazochukuliwa kikanda kama zile za Kamisheni ya Tuna ya Bahari ya Hindi (Indian Ocean Tuna Commission – IOTC). Mfumo wa usimamizi wa FAD unapaswa kuwa na moduli kadhaa, zikiwemo: Ufanisi wa Uvuvi wa Maumbo Yanayowavutia Samaki – FAD, Ufanisi wa Masoko ya Samaki, Uimarikaji wa Ustawi wa Mwanadamu, Ufanisi katika Usimamizi wa Uvuvvi wa FAD (upatikanaji wa FAD na nyenzo zake), Athari za FAD katika kupunguza kiwango na jitihada za uvuvi wa samaki wa karibu na pwani.

3.2.3 KUONGEZA THAMANI KATIKA UVUVI

Katika muktadha wa udhibiti mbaya wa uvuvi, mpango wowote wenye lengo la kuongeza thamani kwenye uvuvi ambao utahusisha kuongeza bei za samaki na kusababisha faida zaidi kwa wavuvi, utachochea zaidi tatizo ambalo tayari lipo la kelemewa au kumalizwa kabisa kwa rasilimali za uvuvi (samaki) katika maji madogo. Aidha, kuongezeka kwa tija ka wavuvi kutachochea tatizo la wavuvi kutozingatia kanuni za uvuvi zilizopo. Kwa hivyo, jitihada za hatua za kuongeza tija katika sekta ya uvuvi zitategemea sana uwezo wa Zanzibar wa kufanya mabadiliko katika taasisi zinazosimamia uvuvi ili ziweze kusimamia kwa ufanisi uvuvi wa maji madogo na hasa ziweze kudhibiti kiwango kikubwa cha na wingi wa wavuvi katika maeneo hayo.

Kutokana na hali hiyo, kuna haja ya kuwepo kwa mfumo wa kuongeza thamani hatua kwa hatua kwa samaki waliokwisha vuliwa, kuunganisha pamoja mipango mengine inayohusiana na jambo hilo kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa uvuvi wa bahari ya karibu na pwani na kuendeleza uvuvi wa mbali na pwani katika bahari yenye kina kikubwa.

Hata hivyo, mipango hii isiathiri hatua zinazochukuliwa ya kupunguza hasara za kiuchumi na upotevu wa samaki waliovuliwa na wanaoweza kuvuliwa. Aidha, mipango hiyo iimarishe usafi wa samaki wakati wanapobebwa, wanapohifadhiwa, na wanapokuwa katika utaratibu wa mauzo masokoni (kwa ujumla kuimarisha ubora wa samaki). Zaidi ya hayo, mipango ya kuongeza thamani katika uvuvi ilenge maeneo ya rasilimali za uvuvi ambazo hazijashughulikiwa ipasavyo, kama vile uvuvi wa kamba ambao hufanywa na wanawake. Soko la kamba linaweza kuongezeka zaidi kutokana na kuongezeka kwa hoteli na mikahawa. Hata hivyo, jambo hilo litafanikiwa endapo usafi utaimarishwa.

Pia kutakuwa na haja ya kuzingatia masuala ya jinsia katika kufanya uchambuzi wa mtiririko wa thamani ili kuhakikisha kwamba jitihada za kuondosha umasikini zinawanufaisha pia wanawake.

3.2.4 MAMBO MENGINE YANAYOPASWA KUIMARISHA KATIKA MFUMO WA UTAWALA ILI KUUFANYA UJITOSHELEZE KWA AJILI KULETA "HALI BORA ZAIDI" KATIKA USIMAMIZI WA SEKTA YA UVUVI

Matumizi ya misingi elekezi yanaelekeza kufanyika kwa mabadiliko katika taasisi na sheria zinazohusika na uvuvi. Lengo la mabadiliko haya ni kuimarisha vipengele muhimu katika mhimili wa sasa wa utawala wa uvuvi. Mabadiliko hayo yanafafanuliwa hapo chini.

Misingi elekezi pia inaelekeza matumizi ya misingi ya utawala bora wakati wa kufasili na kutoa huduma kwa jamii katika sekta ya uvuvi, ikiwemo huduma za usimamizi wa sekta hiyo. Misingi mikuu muhimu ya utawala bora ambayo inapaswa kuzingatiwa kwa kiasi kikubwa ni kama ifuatayo:

Kuimarisha uwazi. Kwa kuzingatia hali za sasa za kitakwimu, elimu ya sayansi na mfumo wa taarifa zilivyo na ili kuimarisha utoaji wa maamuzi na ufuatiliaji na tathmini ya sera za uvuvi, kuna haja ya kuweka mazingira mazuri ya kuimarisha ushirikishwaji na Mpango Shirikishi wa Usimamizi wa Ukanda wa Pwani (ICZM). Pia kuongeza ufanisi katika miundo tafauti ya Uongozi wa Uvuvi.

Kuongeza thamani katika Usimamizi wa Uvuvi. Pamoja na kuelimisha kuhusiana na dhana ya Kanuni ya Kipaumbele cha Kusimamia sheria ipasavyo (Priority Regulation for Strong Enforcement – PSE) kwa ajili Usimamizi na Ufuatiliaji, Udhibiti na Ulinzi (MSC) wa uvuvi wa karibu na pwani, matumizi ya misingi ya utawala bora ambayo ina lengo la kuingeza ufanisi, yanaweza kufikiwa kwa kuongeza ugawanaji wa wazi wa majukumu kati ya Uongozi wa Uvuvi na taasisi nyingine ya usimamizi katika utoaji wa huduma za usimamizi. Kwa upande mwengine, uwepo ugawanaji wa majukumu kati ya serikali na sekta binafsi (Ushirikiano wa Serikali na Sekta binafsi).

Kutokana na maelezo ya hapo juu, kuna haja ya kutoa kipaumbele kwa miradi inayolenga kuleta mabadiliko ya kimuundo na kuunganisha sekta mbali mbali katika usimamizi wa uvuvi wakati wa kutafuat aina ya miradi/hatua zinazopaswa kufanywa kwa ajili ya kuimarisha uhusiano kati ya uongozi wa uvuvi, utafiti, wavuvi, na wadau wengine wa ICZM wakiwemo sekta za utalii, mazingira, serikali za mikoa na Mashirika Yasiyo yaKiserikali (NGOs).

4. VIPENGELE VYA KIMKAKATI VYA KUIMARISHA UTAWALA NA USIMAMIZI WA UVUVI ZANZIBAR

4.1 KUIMARISHA VIPENGELE MUHIMU KATIKA MHIMILI WA UTAWALA WA UVUVI

4.1.1 KUIPITIA NA KUIBADILISHA SERA YA UVUVI YA MWAKA 2000

Sera ya Uvuvi ya mwaka 2000 iliyopitiwa na kufanyiwa mabadiliko inapaswa kuchukuliwa kama waraka muhimu katika Uongozi wa Uvuvi kwa sababu itasaidia utekelezaji wa Mkakati huu. Sera ya Uvuvi pia itashughulikia huduma za jamii ambazo Uongozi wa Uvuvi unawajibika nazo na ambazo hazijaguswa sana na Mkakati huu. Huduma hizi, kwa kiasi kikubwa, ni zile zinazohusiana na kunyanyua ubora wa samaki.

4.1.2 KUSHAJIISHA UKAMILISHAJI NA UPITISHAJI WA VIFUNGU VYA SHERIA YA UVUVI YA MWAKA 2010 VINAVYOSAIDIA UTEKELEZAJI WA MKAKATI

Sheria ya Uvuvi ya Zanzibar Namba 7 ya mwaka 2010 (Sheria ya Uvuvi, 2010) inaifuta Sheria ya Uvuvi ya mwaka 1988, na hivyo kufanya maboresho katika usimamizi na maendeleo ya uvuvi katika Bahari ya Zanzibar pamoja na eneo la ndani la bahari. Mabadiliko madogo ya Sheria ya Uvuvi, hata hivyo, yanahitajika ili kuimarisha utawala wa sekta ya uvuvi, hasa katika maeneo ya Sera yanayowapa viongozi nguvu kubwa za maamuzi. Maeneo hayo ni pamoja na Mipango ya Usimamizi wa Uvuvi (FMP) na kutokuwepo kwa utaratibu wa mashirikiano kati ya taasisi kuu za umma na binafsi katika utoaji wa maamuzi. Hata hivyo, kipaumbele katika kipindi cha muda mfupi na muda wa kati kitakuwa ni kuimarisha utekelezaji wa Sheria mpya, kwa sharti kwamba itasaidia kwa kiasi kikubwa kuimarisha usimamizi wa uvuvi wa karibu na pwani.

Kwa ufupi, hatua hii inahusiana na kukamilisha na kupitisha mswada wa Kanuni za Kitengo cha Hifadhi ya Bahari (MCU), ambazo zitawezesha utendaji kazi wa Mifumo ya utawala wa uvuvi iliyoimarishwa katika Maeneo ya Hifadhi ya Bahari (MCAs).

Hatua hii pia hii inahusiana na kukamilisha na kupitisha Kanuni mpya za Uvuvi zitakazosaidia utekelezaji wa Sheria ya Uvuvi ya mwaka 2010. Miongoni mwa changamoto kubwa zilizopo ni pamoja na kufanyia marekebisho makosa na adhabu (kwa ajili ya kuimarisha utii wa kanuni na sheria) kwa

kuzingatia mtazamo wa Kanuni ya Kipaumbele cha Kusimamia sheria ipasavyo (Priority Regulation for Strong Enforcement – PSE), kwenda sambamba na mabadiliko ya Kimataifa ya hivi karibuni ambayo yameanzisha Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu (DSFA) pamoja na kanuni nyengine zinazowiana na hizo.

4.1.3 KUIMARISHA UFANISI WA UONGOZI WA UVUVI

Hivi karibuni Uongozi wa Uvuvi ulibadilishwa muundo wake kwa lengo la kuleta ufanisi katika sekta ya uvuvi. Mabadiliko makubwa yalikuwa ni kuugawa uongozi wa uvuvi katika idara mbili; idara ya kwanza inayoshughulikia uvuvi (Idara ya Maendeleo ya Uvuvi – Department of Fisheries Development, DFD) na idara ya pili ni ile inayoshughulikia kilimo cha baharini pamoja na matumizi ya samaki (Idara ya Rasilimali za Baharini – Department of Marine Resources, DMR). Hata hivyo kuna kuingiliana kwa mamlaka za baadhi ya vitengo/sehemu miongoni mwa Idara zote mbili, hasa kuhusiana na masuala ya samaki waliokwisha vuliwa. Jambo hili linaathiri ufanisi wa Uongozi wa Uvuvi. Jambo jengine muhimu ni kwamba, muundo wa sasa hauruhusu utenganishaji wa wazi wazi kwa masula yanayohusiana na uvuvi (kwa mfano leseni, kuongeza muda, takwimu na miundombinu), usimamizi za uhifadhi wa mazingira katika uvuvi (kwa mfano, Maeneo ya Hifadhi ya Bahari – MCA, Mipango ya Usimamizi wa Uvuvi – FMP, na Ufuatiliaji wa Uvuvi), na matumizi ya samaki. Aidha, muundo wa sasa hazitowi uhuru wakutosha wa kifedha na utendaji kazi kwa Ufuatiliaji, Udhibiti na Ulinzi (MCS), ambayo kimtazamo ina hadhi ya kiwango cha Idara.

Kutokana na hali hiyo, inapendekezwa kwamba mabadiliko madogo ya kimuundo katika Uongozi wa Uvuvi yafanyike ili kuimarisha ufanisi katika matumizi ya rasilimali chache za umma zilizopo na kuongeza ufanisi wa jumla wa uongozi wa uvuvi.

Uimarishaji wa ufanisi katika uongozi wa uvuvi unapaswa kuzingatia mambo yafuatayo:

- Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi kuhusu usimamizi wa uvuvi na Nyanja nyengine zinazohusana na uvuvi (kama vile mambo ya msingi yakiwemo uelewa wa kanuni pamoja na matumizi yake), hasa kuhusu hatua/mipango mahsusi (yaani kuwa na mafunzo yenye tija na sio kufanya mafunzo ambayo hayatasaidia utekelezaji wa majukumu ya mfanyakazi).

- Kuimarisha uwezo wa nguvukazi (rasilimali watu, kifedha, na utendaji wa kila siku katika kada ya uongozi na kuimarisha mafungamano ya kikazi na kiutendaji kati ya viongozi wakuu wa uvuvi na viongozi wa mikoani (maeneo ya uvuvi).

- Kuimarisha upeanaji wa habari miongoni mwa idara, vitengo na sehemu mbali mbali katika uongozi wa uvuvi.

4.1.4 KUJENGA UWEZO KWA ASASI ZA UVUVI ZA KIJAMII NA BINAFSI

Kuimarika kwa uongozi na utawala wa uvuvi kunahitaji kuwepo maendeleo ya taasisi za kitaifa na kutoka maeneo ya uvuvi, za umma na za binafsi, zinazojishughulisha na uvuvi, halali na zenye ufanisi.

Maendeleo makubwa yamepatikana katika kujega uwezo wa Kamati za Uvuvi za vijiji, katika kiwango cha vijiji, hasa katika Maeneo ya Hifadhi ya Bahari. Hata hivyo, bado kuna haja ya kuendelea kuzijengea uwezo jumuiya hizi za kijamii. Ujengaji wa uwezo unapaswa kujumuisha mafunzo, pengine kwa msaada wa Mashirika Yasiyo yaKiserikali (NGOs), pamoja na kuweka wazi hadhi za jumuiya hizi kisheria na wajibu wake katika usimamizi wa uvuvi. Zaidi ya hayo, zinapaswa kujengewa uwezo wa kujiendeleza zenyewe kifedha. Pia kuna haja ya kuimarisha mfumo wa mashauriano kati ya Kamati za Uvuvi za Vijiji zilizo katika eneo fulani la usimamizi wa uvuvi (kama ghuba, kisiwa kidogo, au katika maeneo ya mto wa bahari) ikiwa mamlaka ya kijiji hayataingiliana na maeneo haya. Pia kuna haja ya kuziunganisha na kuzioanisha kanuni za maeneo husika. Hii itasababisha kufahamika kwa maeneo ya usimamizi wa uvuvi katika.

Katika kiwango cha taifa, hakuna vyama vya wavuvi au wadau wanaoshughulikia sekta ya uvuvi. Hili ni pengo kubwa katika mhimili wa utawala wa uvuvi na hatua zinapaswa kuchukulia ili kuweza kuanzishwa vyama vya aina hiyo ili viimarishe majadiliano kati ya viongozi na wadau wa uvuvi.

4.1.5 KUIMARISHA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA, KIKANDA NA KITAIFA KATIKA SEKTA YA UVUVI

Ushirikiano wa kimataifa na kikanda ni suala la Muungano na tayari kuna utaratibu wa kusaidia kujenga ushirikiano kati ya taasisi za Uvuvi Tanzania na zile za kimataifa na kikanda zenye kazi kama hizo (kama vile IOTC, SWIOFC, FAO/COFI, na CAMFA). Hata hivyo, kuna haja ya kuimarisha ushiriki wa taasisi za uvuvi za Zanzibar katika utaratibu huo, hasa katika mikutano ya kisayansi inayozihusu IOTC na SWIOFC.

Zaidi ya hayo, utaratibu wa mashirikiano kati ya Taasisi za Uvuvi za Zanzibar, Tanzania Bara, na zile za Muungano kama DSFA, na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (Tanzania Fisheries Research Institute – TAFIRI) bado haujaandaliwa pamoja na kuwepo kwa changamoto za uvuvi zinazofanan. Aidha kuna haja ya kuandaa utaratibu mzuri wa mashirikiano ili kutatua matatizo ya usimamizi kwa rasilimali za pamoja kama samaki wadogo wanaopatikana katika bahari za ndani na maeneo ya bahari ya sehemu mbili hizo za Tanzania. Ushirikiano na Tanzania Bara hufanywa zaidi kwa misingi ya dharura maalumu pekee na kuna haja ya kuimarisha mashirikiano hayo na kuufanya utaratibu huo kuwa jambo la kawaida.

Kwa kumalizia, msisitizo unapaswa kuwekwa katika upashanaji wa taarifa na mashirikiano ya kiteknolojia na kisayansi katika mambo yanayozihusu pande zote mbili kama vile usimamizi wa uvuvi wa karibu na pwani, kuanzisha uvuvi wa FAD, kuimarisha takwimu (ikiwemo kufanya uchunguzi wa pamoja) na kuanzisha asasi za kijamii (Kamati za Uvuvi za Vijiji – VFCs kwa Zanzibar na Vitengo vya Usimamizi wa Fukwe – Beach Management Units – BMU- kwa Tanzania Bara) kwa lengo la kusaidia usimamizi wa pamoja wa uvuvi.

Kutakuwa na haja ya kuanzisha Kamati ya ‘Pande mbili’ ya Ushauri wa masuala ya uvuvi kati ya Zanzibar na Tanzania Bara. Kamati hii itasaidia usimamizi wa rasilimali za pamoja kama vile samaki wadogo. Kamati pia itasawazisha kanuni za uvuvi za pande mbili, zinazohusiana na uvuvi wa bahari za ndani za kila upande na maeneo ya bahari ambayo ni sehemu ya pande mbili hizo, ili ziweze kulingana.

4.1.6 KUFANYIA MABADILIKO SHERIA YA UVUVI YA MWAKA 2010 ILI IIMARISHE UTAWALA WA UVUVI (MTAZAMO WA MUDA WA KATI HADI MUDA MREFU)

Sheria ya Uvuvi ya mwaka 2010 inampa Waziri nguvu kubwa ya maamuzi nje ya sheria na haishajiishi matumizi ya misingi mengine muhimu ya utawala wa sheria kama vile ushirikishwaji wa wadau, uwazi, na mwendelezo wa sera za umma. Kwa hivyo, itakuwa ni muhimu kufikiria kufanya marekebisho ya Sheria hiyo ili kuimarisha mfumo wa utawala wa uvuvi Zanzibar.

Kwa kumalizia, mkazo mkubwa unatakiwa kuwekwa katika kushughulikia masuala yafuatayo:

- Kuanzisha Bodi ya Taifa ya Ushauri yenye wawakilishi kutoka taasisi za umma na sekta binafsi ambazo kwa namna moja au nyengine zinashughulikia usimamizi wa uvuvi (utawala wa uvuvi, utafiti, Ufuatiliaji, Udhibiti na Ulinzi (MCSs), usalama baharini, mazingira, utalii, serikali za vijiji, wavuvi, na wadau wengine). Taasisi hizi zitakuwa na mamlaka ya kutoa mapendekezo kwa Wizara kwa lengola kusaidia utoaji wa maamuzi yanayohusiana na masuala muhimu (kama kupitia na kufanyia mabadiliko Mipango ya Usimamizi wa Uvuvi

(FMPs), kuanzisha Maeneo ya Hifadhi ya Bahari (MCAs), kupitisha mpango wa Utoaji leseni n.k.).

- Majukumu ya Waziri anayeshughulikia uvuvi kusimamia na kuchapisha mfumo wa taarifa za uvuvi
- Kutambua haja ya kuimarisha mashauriano, kama vile mashauriano na Kamati za Uvuvi za Vijiji (VFCs) na Kamati za Mwani za Vijiji (VSFCs) ili kusaidia utoaji wa maamuzi na kushajiisha ushirikiano kati ya serikali na sekta binafsi katika utoaji wa huduma muhimu za usimamizi wa uvuvi.
- Kuimarisha kazi za Mfuko wa Maendeleo na Usimamizi wa Uvuvi uliopo ili kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji endelevu wa fedha kwa ajili ya kutoa huduma katika sekta ya uvuvi, hasa katika Maeneo ya Hifadhi ya Bahari (MCAs).

4.2 KUIMARISHA UTOAJI WA HUDUMA MUHIMU ZA UVUVI

4.2.1 KUFANYIA MAREKEBISHO MFUMO WA TAKWIMU NA UTOAJI TAARIFA

Mfumo wa sasa wa takwimu ulifanyiwa uchambuzi hivi karibuni na wataalamu wan je. Miongoni mwa mapungufu yaliyobainishwa ni watu wanaofanya kazi ya kurekodi taarifa maeneo ya fukwe kutofuata utaratibu maalumu uliowekwa wa kukusanya taarifa (data), utaratibu usiotosheleza wa kuongeza data na mfumo wa utoaji wa taarifa, na maelezo hafifu kuhusiana na idadi ya samaki wanaopatikana na idadi ya wavuvi waliopo. Mfumo huu pia hauwezi kubainisha uchangamani wa kiakiolojia katika uvuvi wa Zanzibar. Kwa hiyo, mfumo hauwezi kusaidia katika utoaji wa maamuzi kuhusu usimamizi wa uvuvi.

Kuna haja ya kuufanyia mabadiliko mfumo uliopo wa takwimu ili uweze kushughulikia kikamili matatizo yote yaliyotajwa. Hali hii inahitaji uanzishwaji na utekelezwaji wa mradi maalumu wa kusimamia mfumo wa takwimu. Pia kuna haja ya kuhakikisha kwamba takwimu za uvuvi za kila mwaka zinachapishwa.

4.2.2 KUENDELEA KUIMARISHA UDHIBITI NA ULINZI KATIKA UVUVI

Katika muongo uliopita, Zanzibar imepiga hatua kubwa katika kutoa huduma za kuridhisha za udhibiti na ulinzi katika hatua za ulinzi, hasa katika Maeneo ya Hifadhi ya Bahari (MCAs). Hii imesababisha kuongezeka kwa wafanyakazi, fedha na majukumu kwa Sehemu ya ufuatiliaji, Udhibiti na Ulinzi (MCS) katika Idara ya Maendeleo ya Uvuvi (DFD), na hatimaye kuwepo kwa mfumo wa mashirikiano kati ya Wizara inayoshughulikia na Uvuvi na Taasisi nyengine zinazoshughulikia MCS na usalama baharini. Miongoni mwa taasisi hizo ni KMKM na DSFA. Wizara inayoshughulikia Uvuvi inaweza pia kuanzisha ushirikiano mzuri na Polisi na Mfumo wa Mahakama (ikiwemo katika masula ya mashtaka).

Hata hivyo, ufanisi wa mfumo wa MCS unategemea sana ufadhili wa nje na haujaweza kujiendeleza bila ya kuwepo kwa miradi. Hali hii inasababisha kuwepo kwa haja ya kufanya mabadiliko ya kitaasisi katika Uongozi wa Uvuvi ili kuhakikisha kwamba Ufuatiliaji, Udhibiti na Ulinzi (MCS) vinaimarika, kufanikiwa na kuwa endelevu. (Angalia pia 4.1.3).

Changamoto nyengine muhimu ambazo zinapaswa kuangaliwa kwa makini ni kuimarisha udhibiti na ulinzi wa uvuvi, ikiwemo kuwepo kwa mipango mipaya ya utendaji, mfumo mbaya wa mawasiliano ya ndani ya Uongozi wa Uvuvi, kutokuwepo kwa boti za kutosha za kufanyia doria kwa ajili ya usalama bahari, na kutokuwepo kwa mfumo wa taarifa za kipelelezi katika MCS. Aidha kuna umuhimu ya kuzingatia suala la mashirikiano kati MCS na DSFA ya Tanzania Bara.

Zaidi ya hayo, inapendekezwa kwamba mipango ya utekelezaji wa MCS ilenge zaidi Maeneoya Hifadhi

ya Bahari (MCAs) kwa mujibu wa mtazamo wa PSE.

4.2.3 KUWEKA MFUMO BORA WA UTAFITI WA UVUVI

Mfumo mzuri wa utafiti wa uvuvi, kimsingi, unatakiwa kuwa na mfumo utakaoweza kutoa taarifa za kiwango cha rasilimali za bahari (samaki) na mfumo wao wa mazingira ya kiekiololojia. Mfumo huo pia unatakiwa kufahamu aina kuu mbali mbali za uvuvi kwa mujibu vipengele vya kibaiolojia na kiakiolojia, kijamii na kiuchumi, na kutoa ushauri wa kisayansi kwa ajili ya utoaji wa maamuzi, kwa mujibu wa kanuni za kiutawala na kisheria zilizopo. Pamoja na kuwepokwa taasisi mbali mbali za kitaaluma na Mashirika Yasiyo yakiserikali au hatua mbali mbali zinazochukuliwa na Kitengo cha Utafiti cha Wizara inayoshughulikia mifugo, mfumo wa utafiti bado haujaweza kufikia uwezo wa kushughulikia masuala yaliyotajwa hapo juu.

Ili kuondosha mapungufu yaliyomo katika mfumo wa sasa wa utawala wa uvuvi, inapendekezwa kwamba Kitengo cha Utafiti cha Wizara ya Mifugo na Uvuvi Zanzibar kiimarishwe ili kukuza mfumo wa tafiti za uvuvi Zanzibar. Kitengo cha Utafiti kilianzishwa kama Kitengo cha Utaalamu kinachoshughulikia utafiti wa mifugo na uvuvi chini ya Idara ya Mipango , Sera na Utafiti. Kitengo cha Utafiti kina Kamati ya Kitaalamu ya Utafiti ambayo ina mamlaka na uwezo wa kutekeleza programu za kisayansi zinazoshughulikia uvuvi. Katika utekelezaji wa kazi hizo Kitengo hushirikiana na Taasisi ya Sayansi ya Bahari ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Institute of Marine Science – IMC), Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (The State Univerity of Zanzibar – SUZA), na Chuo Kikuu cha Zanzibar (Zanzibar University – ZU). Kamati ya Kitaalamu ya Utafiti inaweza pia kuanzisha vikundi vya utafiti katika nyanja mbali mbali za utafiti. Ili kuhakikisha kwamba Kitengo cha Utafiti kinatoa mchango mkubwa katika kuendeleza mfumo bora wa utafiti wa uvuvi, inapendekezwa kwamba Mratibu mwenye uzoefu wa masuala ya Sayansi ya Uvuvi ateuliwe ili aweze kusaidia na kuratibu kazi za Kamati ya Kitaalamu na Utafiti zinazohusiana na uvuvi.

Changamoto kubwa inayohusiana na kuimarisha Kitengo cha Utafiti ni kuimarisha elimu ya sayansi ya uvuvi inayohitajika kwa masuala mbali mbali yanayohusu uvuvi, hasa mbinu zisizo za moja kwa moja za tathmini na shughuli za utafiti wa kimatumizi kwa ajiliya kusaidia utoaji wa maamuzi katika uongozi wa uvuvi. Changamoto nyengine ya kuimarisha Kitengo cha Utafiti ni kusaidia, kuunganisha na kutangaza jitihada za utafiti wa uvuvi Zanzibar. Pia ni vyema kusisitizwa kwamba Utafiti wa kimatumizi ujumuishe shughuli zinazokusudia kuimarisha mikakati kuzifanya jamii za wavuvi kwenda sambamba na mabadiliko ya tabia nchi.

Kwa malengo ya muda mrefu, na kwa mujibu wa mamlaka iliyonayo, Kitengo cha Utafiti kinaweza kuanzisha chombo maalumu cha utafiti wa uvuvi kitachokuwa chini ya Wizara inayoshughulikia uvuvi.

Aidha, hatua kadhaa zinapaswa kuchukuliwa kwa kipindi cha muda mfupi na muda wa kati katika kuendeleza mfumo mzuri wa utafiti wa uvuvi. Miongoni mwa hatua hizo ni kama zifuatazo:-

- Kuanzisha Mikataba ya Mashirikiano (Memorandum of Understanding – MoU) kwa lengo la kushirikiana na kushughulikia data kati ya Kitengo cha Utafiti na Uongozi wa Uvuvi.
- Kutafuta na kutekeleza mpango wa mafunzo ya utafiti ya msingi na ya kiwango cha juu kwa watafiti.
- Kuweka orodha ya mahitaji ya vipaumbele vya utafiti na kuanzisha mpangp wa pamoja wa utafiti utakaojumuisha taasisi za umma (kama Kitengo cha Utafiti cha Wizara ya Mifugo na Uvuvi) na Taasisi za watu binafsi (Mashirika Yasiyo yaKiserikali – NGOs).
- Kwa kupitia mwavuli wa Kitengo cha Utafiti cha Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kuandaa kikundi kazi cha kisayansi kitakachoshughulikia uvuvi Zanzibar kila baada ya miaka 4 au 5 ambacho kitazileta pamoja Taasisi mbali mbali kama SUZA, Taasisi za Tanzania Bara

kama TAFIRI, Taasisi za Muungano kama IMS, DSFA na ikiwezekana Taasisi za kikanda kama SWIOFC, IOTC na WIOMSA.

- Kuandaa utaratibu wenye lengo la kuhakikisha kwamba kuna maoni ya mara kwa mara kutoka kwa jamii za wavuvi kuhusiana na matokeo ya tafiti.

4.2.4 KUANDAA MFUMO WA TAARIFA ZA UVUVI

Kazi kuu ya mfumo wa taarifa za uvuvi ni kuimarisha utoaji wa maamuzi, kuongeza ufanisi wa taasisi za umma na binafsi, kujenga mazingira mazuri ya kuimarisha ushirikishwaji na utii wa sheria wa hiari, na kuchangia katika kupunguza uingiliaji wa kisiasa kwa kuimarisha utawala na usimamizi wa sekta ya uvuvi. Mfumo wa taarifa za uvuvi upatiwe data kutoka taasisi mbali mbali (ikiwemo uongozi wa uvuvi, na nyenginezo). Mfumo huo uwe na moduli tatu, ambazo ni:

- Mhimili wa Usimamizi wa Uvuvi – data na taarifa kuhusiana na taasisi zinazoshughulikia uvuvi, sera, sheria, kanuni, Mpango Mkuu wa Usimamizi (GMP) wa Maeneo ya Hifadhi ya Bahari (MCAs), Mpango wa Usimamizi wa Uvuvi (FMP), miradi ya maendeleo n.k.

- Hali ya Sekta ya Uvuvi – data na taarifa kuhusu hali ya maliasili za uvuvi, ukubwa wa chhombo cha uvuvi, idadi wa wavuvi, idadi ya leseni (boti, wavuvi na wahusika wengine), kesi za uvunjaji wa sheria, idadi ya adhabu, maeneo ya masoko n.k.

- Ufanisi wa sekta ya uvuvi kwa mujibu wa maendeleo ya kijamii na kiuchumi na utunzaji mazingira – data na taarifa ziwe zinahusu uchambuzo wa mlolongo wa thamani, matumizi ya samaki, aina za mimea na samaki wanaopatikana baharini.

4.2.5 UFUATILIAJI NA TATHMINI YA MKAKATI WA UTAWALA WA UVUVI

Kuna haja ya kuwepo kwa ukubalifu, utayari na kutumia fursa zilizopo katika utekelezaji wa Mkakati wa Utawala wa Uvuvi. Kwa kumalizia, ufuatiliaji na tathmini ya mara kwa mara inahitajika kufanyika kwa kutumia viashiria vilivyochaguliwa kwa uangalifu.

Pia, ni muhimu kuandaa warsha ya wadau tafauti kila baada ya miaka 3 kwa lengo la kutathmini kiwango cha utekelezaji wa Mkakati wa utawala wa Uvuvi na kupendekeza mabadilikoyanayopaswa kufanywa.

4.3 KUZIFANYA SHUGHULI ZA UVUVI NA NYENGINE ZINAZOLINGANA NA UVUVI KUWA RASMI NA ZA KITAALAMU

4.3.1 KUWEKA MASHARTI YA CHINI YA KURUHUSIWA KUVUA

Kanuni za Usafiri wa Majini (Usajili na Leseni za Vyombo vya baharini) za mwaka 2007 na Sheria ya Uvuvi ya mwaka 2010 zinatoa masharti ya chini ya usajiliwa vyombo vya uvuvi, utoaji wa leseni kwa chombo cha uvuvi na utoaji wa leseni kwa wavuvi na watu wengine wanaofanya kazi zinazohusiana na uvuvi. Hata hivyo, pamoja na kuwepo kwa masharti ya kisheria na gharama ndogo kwa wavuvi na wahusika wengine wa aina (gharama za leseni ni ndogo sana), shughuli nyingi za uvuvi zinafanywa kwa njia zisizo rasmi.

Uanzishaji wa masharti ya chini kabisa, ambapo mvuvi akiyakamilisha anaruhusiwa kuvua, itakuwa ni hatua moja kubwa ya kuimarisha utawala na usimamizi wa uvuvi Zanzibar. Hii itakuwa ni hatua ya kwanza ya katika kudhibiti idadi ya wavuvi na kuelemewa kwa sekta ya uvuvi. Utaratibu wa usajili na utoaji leseni uanze haraka iwezekanavyo na ufanywe kwa mashirikano ya karibu kati ya Idara ya Maendeleo ya Uvuvi (DFD), Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar (ZMA), Afisa Uvuvi wa Wilaya

(DFOs) na wavuvi kupitia Kamati za Uvuvi za Vijiji (VFCs). Shughuli za kufanya ni kama zifuatazo:

- Kutoa taarifa na kuongeza uelewa kwa wavuvi, (wa aina zote mbili; wakaazi na wahamiaji) pamoja na wahusika wengine wa sekta ya uvuvi, kufuata taratibu za usajili na leseni.
- Kuongeza uwezo kwa wafanyakazi wa Idara ya Maendeleo ya Uvuvi ili waweze kushughulikia masuala ya leseni.
- Kuanzisha na kusimamia mfumo wa kompyuta wa hazinadata (dabase) wa masuala ya usajili na leseni katika kiwango cha Idara ya Maendeleo ya Uvuvi.
- Kuzingatia, na ikibidi kutekeleza, utaratibu wa usajilikwa na ukataji leseni kwa kutumia simu za mkononi zinazotumia mitandao iliyo nchini. Utaratibu huu kwa sasa unafanyiwa majaribio huo Tanzania Bara na maeneo mengine ya ukanda huu.

4.3.2 KUKAMILISHA NA KUTEKELEZA BANDARI RASMI ZA UVUVI

Sheria ya Uvuvi ya mwaka 2010 inaelekeza kuanzishwa kwa bandari za uvuvi na Uongozi wa Uvuvi kwa mashaurino na Taasisi za Serikalizinazohusika. Hii, inaaminika, itasaidia sana kuifanya sekta ya uvuvi na shughuli zinazohusiana na uvuvi kuwa rasmi na kuwaya kitaalamu. Hivyo, jitihada za uanzishaji wa bandari hizo zinapaswa kuendelezwa.

4.3.3 KUIMARISHA MIKAKATI YA KUNYANYUA HALI ZA MAISHA ZA JAMII ZA WAVUVI (KWA KUTOA KIPAUMBELE KWA KIZAZI KIPYA)

Kuelekea wavuvi wa kisasa na walioelimika

Ili kupunguza migogoro ya kimaslahi kati ya wadau kutoka serikalini na wale wa sekta binafsi katika suala la kuhakikisha kuwa rasilimali za uvuvi zinaendelea kuwepo, kuna haja ya kujenga mazingira yatakayoruhusu kuwepo kwa majadiliano. Kuanzishwa kwa vyama vya wavuvi vya kitaifa, kama ilivyoelezwa hapo juu, kutasaidia kufikiwa kwa lengo hili. Changamoto nyengine iliyopo ni ya kuanzisha jitihada za kuimarisha kiwango cha uvuvi ili kiwe cha kitaalamu (uvuvi wa kisasa) katika masuala elimu waliyonayo wavuvi, pamoja na utaalamu na ujuzi wao wa uongozi. Kwa hivyo, itakuwa ni jambo muhimu sana kushughulikia masuala ya elimu na uelewa wa wavuvi hasa kwa kuwekeza katika vizazi vijavyo. Wizara inayosimamia sekta ya uvuvi, kupitia chuo chake kitakachoanzishwa hapo baadaye inapaswa kutoa mchango mkubwa katika kufanikisha jambo hili. Washirika wa maendeleo pamoja na Wizara ya elimu na Mashirika Yasiyo yaKiserikali (NGOs) zifikiriwe kama wadau muhimu wa kufanikisha mpango huu.

Kuimarisha ushirikiano wa Jamii za wavuvi katika programu za kijamii

Kutokana na maeneo wanayoishi wavuvi kuwa mbali, jamii hizi zimekuwa zikishindwa kunufaika ipasavyo na programu na huduma za kijamii ikiwemo elimu ya msingi na afya (kama vile mafunzo kuhusu VVU/UKIMWI). Ni vyema ukawekwa msisitizo kwamba programu za kielimu zainaweza kuongeza uwezo wa jamii za pwani kujishughulisha na kazi nyengine za kujiongezea kipato mbalina uvuvi, jambo ambalo linaweza kuwa ni njia mojawapo ya kuondoa tatizo la kuelemewa kwa sekta ya uvuvi katika maeneo ya bahari ya karibu na pwani. Kwa hiyo, kuna haja ya kusaidia mipango yenye lengo la kuimarisha ongezeko la jamii za wavuvi katika programu za kijamii zinazoendeleshwa na serikali, washirika wa maendeleo na Mashirika Yasiyo yaKiserikali (NGOs).

Kutatua Migogoro katika Uvuvi

Migogoro kadhaa inayohusiana na suala la uvuvi imetokea Zanzibar. Migogogro hiyo imesababishwa na mambo mbali mbali kutegemeana na eneo lilipotokea mgogoro na jamii zilizohusika na mgogoro huo. Miongoni mwao ni migogoro inayohusiana na utunzaji wa mazingira, matumizi ya vifaa tafauti vya kuvulia kwa wakati mmoja, wavuvi wahamiaji, shughuli za utalii na kati ya ukulima wa mwani na uvuvi. Vyanzo vya migogoro hii, kwa jumla, havieleweki vyema miongoni mwa jamii. Kwa hiyo, kuna haja ya kunyayua uelewa wa wavuvi kuhusina na vyanzo vya migogoro. Aidha, kuna haja ya kutungwa kwa sheria ndogo ndogo ili kusaidia utaratibu wa asili wa kutatua migogoro.

Kuimarisha mikakati wa kwenda sambamba na mabadiliko ya tabia nchi

Tabia nchi ina athari mbali mbali za hali ya mazingira, wanyama na mimea katika uvuvi wa bahari ya karibu na pwani, ikiwemo maeneo ya fukwe yenye kingo za miamba. Athari kamili ya mabadiliko ya hali nchi bado hayajafahamika ipasavyo na kuna haja ya kuanzisha programu nzuri za utafiti. Kwa sasa, kuna haja ya kuongeza uelewa kwa serikali za vijiji na NGOs kuhusiana na suala la mabadiliko ya tabia nchi na kuanzisha programu kubwa kuwawezesha wavuvi na wakulima wa kilimo cha baharini kwenda sambamba na mabadiliko hayo.

4.4 KUIMARISHA USIMAMIZI WA UVUVI WA MAENEO YA BAHARI YA KARIBU NA PWANI

4.4.1 KUIMARISHA UFANYAJI KAZI NA USIMAMIZI WA MAENEO YA HIFADHI YA BAHARI (MCAs)

Kuna nyenzo kadhaa za kisera, kisheria na za udhibiti za kusaidia uhifadhi wa mazingira Zanzibar. Miongoni mwa nyenzo za kisheria za kusimamia Maeneo ya Hifadhi ya Bahari (MCAs), kwa sasa, ni Sheria ya Uvuvi ya mwaka 2010 ambayo inaelekeza undaaji wa Kitengo cha Hifadhi ya Bahari (MCU). Sheria ya Uvuvi ya mwaka 2010, hata hivyo, itatekelezekakwa ukamilifu wakati mswada wa kanuni za MCU utakapokamilika na kupitishwa baada ya mashauriano na wadau mbali mbali. Madhumuni ya kanuni za MCU ni kupendekeza mhimili mmoja wa kisheria utakaochukua nafasi ya Amri za MCAs na kuimarisha utawalawa Maeneo ya Hifadhi ya Bahari (MCAs).

Pia kuna haja ya kuimarisha nguvu kazi na uwezo katika Kitengo cha Hifadhi ya Bahari kwa ajili ya kusaidia utendaji kazi wa Maeneo ya Hifadhi ya Bahari (MCAs). Hatua hii itajumuisha kuongeza rasilimali watu na fedha ilikuhakikisha kwamba MCU zinafikia lengo na wajibu wake wa kuratibu uhifadhi wa Maeneo yote ya Hifadhi ya Bahari Zanzibar.

Pia, kila moja kati ya maeneo matatu ya Hifadhi ya Bahari yaliyowekwa (PECCA, MIMCA, na MBCA) yameunda Mipango Mikuu ya Usimamizi (GMPs) kwa lengo la kusimamia uvuvi. Mipango hiyo imeshapitishwa na itakuwa ni nyaraka rasmi za mipango wakati mswada wa Kanuni za Kitengo cha Uhifadhi wa Bahari zitakapopitishwa. Hii pia itasaidia utendaji kazi wa Maeneo ya Hifadhi ya Bahari, iwapo fedha za kutosha zitapatikana.

Mwisho, kuna haja ya kuhakikisha kwamba hatua maalumu za usimamizi ndani ya MCAs zenyewe zinatafutwa na kutayarishwa kwa kuzingatia ushihidi mdogo wa kisayansi na kwa mujibu mtazamo wa PSE. Lengo la hatua hizo ni kuongeza ufanisi.

4.4.2 KUIMARISHA MBINU YA KANUNI YA KIMAUMBILE YA KUSIMAMIA SHERIA KWA UVUVI WA BAHARI YA KARIBU YA PWANI , NJE YA MAENEO YA HIFADHI YA BAHARI (Priority Regulation for Strong Enforcement – PRSE)

4.4.3 Istilahi na misingi elekezi muhimu inayohusiana na Kanuni za Kipaumbele cha Kusimamia

sheria ipasavyo (PSE) zimeshaelezwa hapo juu katika sehemu ya 3.2.1. Katika warsha iliyofanyika mwanzoni mwa Desemba 2013, **washiriki** waliombwa kuandaa Kanuni za Kipaumbele kwa kutumia vigezo tafauti. Kanuni za Kipaumbele sita (6) nje ya Maeneo ya Hifadhi ya Bahari ziliainishwa. Kanuni hizi ni zile zinazohusu uvuvi wa kukokoteza nyavu katika maeneo ya miamba ya matumbawe, saizi ya matundu ya nyavu, kutanda samaki katika maeneo nyeti, kutumia bunduki za mishale, matumizi ya nyavu za kamba moja, na matumizi ya milipuko na sumu. Uchunguzi zaidi uhahitajika kuandaa orodha ya mwisho ya kanuni za kipaumbele. Uchunguzi huu ufanyike kwa mashirikiano na wavuvi, kwa sababu vipumbele vinaweza kubadilika kutegemea na eneo la uvuvi, kwa mfano katika baadhi ya maeneo kipaumbele cha matumizi ya nyavu zenye matundu madogo kinaweza kuhitajika zaidi kuliko maeneo mengine. Hata hivyo, orodha ya awali iliyopatikana inapaswa kizingatiwa wakati wa uundaji wa kanuni za mwisho. Hii ni kwa sababu mafanikio ya matumizi ya mbinu za PSE utategemea sana kukubaliwa kwa idadi ndogo tu ya kanuni za kipaumbele (yaani kwa wingi ziwe kanuni 5 au 6). Aidha, utekelezaji wa mpango wa PSE utategemea na hatua zifuatazo:

- Uchoraji wa ramani za maeneo ya uvuvi nje ya Maeneo ya Hifadhi ya Bahari (MCAs) kwa lengo la kufahamu maeneo gani nyeji ambapo uvuvi wa kutanda utapigwa marufuku moja kwa moja.
- Kuongeza uelewa na mashauriano na wavuvi (wakaazi na wahamiaji) na wahusiaka wengine wa masuala ya uvuvi kuhusu PSE.
- Kutafuta adhabu na vikwazo vinavyofaa ili kuzuia kwa kuongezeka uvunjaji wa Kanuni za Kipaumbele, na kuziingiza katika kanuni za uvuvi.
- Kuhakikisha kwamba mipango ya utekelezaji wa Ufuatiliaji, Udhibiti na Ulinzi (MCS) inazingatia mbinu ya PSE
- Kuongeza uelewa kwa serikali za vijiji na taasisi kadhaa katika maeneo husika zikiwemo Polisi na Mahakama kuhusu changamoto zinazohusiana na mbinu za PSE
- Kuwepo taarifa na mawasiliano ya mara kwa mara kuhusiana na utekelezaji wa PSE, ikiwemo taarifa za utii ya kanuni bila shuruti, kesi za uvunjifu wa kanuni, na adhabu.

4.4.4 KUIMARISHA MIPANGO YA USIMAMIZI WA UVUVI (FISHERIES MANAGEMENT PLANS – FMPs) KATIKA AINA ZA UVUVI ZINAZOPEWA KIPAUMBELE

Kwanza kabisa, usimamizi wa uvuvi una lengo la kuhakikisha kwamba kuna uwiano endelevu baina ya rasilimali za uvuvi na kazi zenyewe za uvuvi zinazofanywa pamoja na kunyanyua, kwa jumla, hali ya kijamii na kiuchumi katika shughuli za uvuvi na shughulli nyengine zinazohusiana nazo. Aidha, usimamizi wa uvuvi unalenga kusaidia kufikiwa kwa malengo mengine ya kijamii kama usimamizi wa maeneo ya pwani. Usimamizi wa uvuvi Zanzibar hadi sasa umekuwa ukishughulikia zaidi kuimarisha sekta hiyo kwa kutumia mhimili mkuu wa kanuni za uvuvi, ikiwemo matumizi ya hatua za kitaalamu za kuhifadhi na kulinda Maeneo ya Hifadhi ya Bahari (MCAs). Kwa sasa, suala la wavuvi kuvua bila kikwazo chochote na watu wengi kuvua katika maeneo mamoja halijashughulikiwa.

Zanzibar kwa sasa ipo tayari kuimarisha mipango ya usimamizi wa uvuvi (FMPs) ili kushughulikia baadhi ya mapungufu hayo. Mpango wa usimamizi wa Uvuvi (Fisheries Management Plan – FMP) ni aina maalumu ya uvuvi ambayo kwa kawaida hujikita katika aina fulani ya/za samaki. Mpango huu huimarisha mhimili mkuu wa kanuni za uvuvi kwa kutumia hatua mahsusi za usimamizi wa uvuvi, kama vile hatua zinazohusiana na kanuni za uhuru wa kuvua. Vile vile huwawezesha wasimamizi kufanya marekebisho madogo madogo katika malengo ya usimamizi ili waweze kushughulikia kwa ufanisi ongezeko la thamani katika sekta ya uvuvi. Mipango ya Usimamizi wa Uvuvi pia ni nyenzo muhimu ya usimamizi ambayo huongeza ushirikishwaji wa wadau katika usimamizi huo, na hatimaye kuongeza ufanisi kwa sekta ya umma na sekta binafsi. Ufanisi huu husababishwa na athari zinazopatikana kutokana na kufanyiwa mabadiliko mipango ya usimamizi wa uvuvi (kama vile utoaji wa huduma muhimu kama ukusanyaji wa data, kufanya tafiti na kuimarisha Ufuatiliaji, Udhibiti na Ulinzi (MCS) kwa

mujibu wamatakwa ya Mpango wa Usimamizi wa Uvuvi – FMP).

Uzoefu katika bara la Afrika unaonesha kwamba ili Mipango ya Usimamizi wa Uvuvi (FMPs) ifanikiwe ni lazima izingatie utaratibu wa kuimarisha utawala na usimamizi wa uvuvi, na utaratibu huo uwe na hatua mbili (2) tafauti lakini zinazosaidiana. Hatua ya kwanza (ya muda mfupi hadi mrefu) ilenge kuainisha aina mbali mbali zinazofaa za usimamizi kwa mujibu wa aina za uvuvi na ifanye mabadiliko ya kitaasisi ambayo yataruhusu Mipango mipya ya baadaye ya usimamizi wa uvuvi kuweza kukubalika na kutekelezeka bila ya matatizo. Kwa hiyo, hatua ya kwanza ilenge katika kubadilisha mfumo wa usimamizi wa uvuvi, na kwa mujibu wa mtazamo wa utekelezaji wa Mpango wa usimamizi wa uvuvi. Hata hivyo, hatua hii inaweza kuanzisha hatua za kitaalamu za usimamizi (kama vile misimu ya kuzuia uvuvi) na hatua za kijadi zilizopo. Hatua ya pili (ya muda wa kati hadi muda mrefu) ishughulikie utekelezaji na upitiaji upya wa toleo la mwisho la Mpango wa Usimamizi wa Uvuvi.

Utiliaji mkazo wa vipengele vya kisayansi vilivyotajwa na kutokuwepo kwa tafauti ya wazi kati ya hatua mbili hizo vinaweza kupelekea kupatikana kwa maendeleo madogo ya Mipango ya Usimamizi wa Uvuvi katika ukanda huu. Mambo mengine muhimu yanayosaidia maendeleo ya FMPs ni haja ya kuweka uwazi kazi za kitengo cha usimamizi wa uvuvi (kwa mfano Mpango wa Usimamizi wa Uvuvi wa Kitaifa ambao unahusiana na rasilimali za pamoja za uvuvi unaweza kusababisha kutopatikana kwa ufanisi wa kutosha ikiwa utaratibu wa ushirikiano hautatayarishwa). Jambo jengine ni haja ya kuanzisha na kuimarisha hatua kwa hatua idadi ndogo ya 'vipaumbele' vitakavyopatikana kwa kuzingatia hali za kibaiolojia, kiekiolojia, kijamii na kiuchumi pamoja na vigezo vya vinavyohakikisha uwezekano wa mipango hiyo kutekelezeka. Zaidi ya hayo, Mipango ya Usimamizi wa Uvuvi ni michakato changamani na yenye gharama, kwa hiyo kuna haja ya kuzingatia sana matumizi ya kanuni ya ufanisi kwa Mipango ya mwanzo ya Usimamizi wa Uvuvi (yaani ubora kwa mujibu wa gharama katika usimamizi wa uvuvi). Mwisho, ni muhimu sana, wakati wa kuandaa Mipango ya Usimamizi wa Uvuvi (FMPs) kuzingatia masuala yanayohusiana na mafunzo na kuongeza uwezo na kuwashirikisha wataalamu waliobobea katika fani husika, ambao kwa sasa hawapatikani Zanzibar.

Kutokana na yote yaliyoelezwa hapo juu, inapendekezwa kwamba kuimarisha Mipango ya Usimamizi wa Uvuvi katika vipeumbele mahsusi vya uvuvi kunahitaji hatua mbili tafauti. Hatua ya kwanza (ya muda mfupi hadi muda wa kati), Mipango ya Usimamizi wa Uvuvi izingatie hatua zenye lengo la kubadilisha mfumo wa utawala na usimamizi wa uvuvi uliopo. Hatua ya pili (ya muda wa kati hadi muda mrefu) izingatie utekelezaji (na ikibidi kuifanyia mabadiliko) Mipango ya mwisho ya usimamizi wa Uvuvi.

4.4.5 KUENDELEZA UTEKELEZAJI WA MIPANGO YA UHIFADHI WA MAZINGIRA YA MAENEO YA PWANI (ICMZ)

Taasisi inayoongoza uhifadhi wa maeneo ya pwani ni Wizara inayoshughulikia mazingira. ICZM inahusisha pia taasisi nyengine za umma zikiwemo Wizara inayoshughulikia Uvuvi na Wizara inayoshughulikia Misitu (usimamizi wa mikoko) pamoja vikundi vya kijamii na taasisi binafsi (ushirika, NGOs). Mswada wa Mkakati wa Uhifadhi wa Mazingira wa Maeneo ya Pwani na Mpango wa Utekelezaji viliundwa mwaka 2009. Pia ni vyema ieleweke kwamba mswada huo unataja masuala kadhaa yanayohusu uimarishaji wa usimamizi na uhifadhi wa rasilimali za bahari. Hatua muhimu zilizotajwa katika mswada huo ni pamoja na kuimarisha Ufuatiliaji, Udhibiti na Ulinzi (MCS), kuongeza ushirikishwaji wa jamii katika usimamizi wa sekta ya uvuvi, kuimarisha uwezo wa kitaasisi, kuimarisha utafiti, na kuendeleza Maeneo ya Hifadhi ya Bahari (MCAs).

Kuna haja ya kuendeleza utekelezaji wa ICM ili kuwafaidisha watumiaji mbali mbali wa mazingira ya pwani, wakiwemo wavuvi, kwa kuimarisha mashirikiano ya kitaasisi na idara nyengine. Kwa mfano panahitajika kusaidia hatua za kushiriki katika uhifadhi wa mazingira (kwa mfano upandaji na uhifadhi wa mikoko na majani ya baharini, usafishaji mzuri wa mitaro ya maji machafu, na kuimarisha sheria ya mazingira) kwa kushirikiana na Wizara zinazoshughulikia misitu na mazingira. Pia kuna haja ya

kusaidia kuongeza uelewa wa jamii za watu wa pwani ndani na nje ya Maeneo ya Hifadhi ya Bahari (MCAs).

4.4.6 KUIMARISHA MFUMO WA KITAIFA WA KUZUIA NA KUPAMBANA NA UCHAFUZI WA MAZINGIRA YA BAHARI

Zanzibar imeanzisha mipango kadhaa yenye lengo la kuhifadhi mazingira ya ukanda wa pwani dhidi ya Uchafuzi wa Mazingira ya Bahari (Marine Pollution – MARPOL) chini ya usimamizi wa jumla wa Idara ya Maafa iliyo chini ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais Zanzibar. Hii inahusisha utayarishaji wa mpango wa dharura wa kupambana na uchafuzi wa mazingira. Ubora na ufanisi wa mfumo huu wa kitaifa unategemea zaidi mashirikiano na taasisi zote ambazo kwa namna moja au nyengine zinashughulika na bahari. Miongoni mwa taasisi hizo ni Wizara inayohusika na Uvuvi (Mfano vyombo vya doria kwa ajili ya Ufuatiliaji, Udhibiti na Ulinzi (MCS). Kwa kuzingatia kwamba uchafu wowote mkubwa wa mazingira ya pwani utakuwa na athari kwa sekta ya uvuvi, kuna haja ya kulipa umuhimu mkubwa suala la uchafuzi wa mazingira ya bahari, hasa katika Maeneo ya hifadhi ya Bahari (MCAs).

4.4.7 KUIMARISHA USIMAMIZI WA UVUVI WA BAHARI YA KARIBU NA PWANI KATIKA MPANGO WA MUDA WA KATI MPAKA MUDA MREFU

Katika kipindi cha muda wa kati na muda mrefu, Mkakati huu utaegemea zaidi katika kuimarisha uwezo wa kitaasisi na mhimili wa kisheria ili kudhibiti kiwango cha jumla cha uvuaji wa samaki, kuimarisha usimamizi ya maeneo yanayodhibitiwa kwa sasa, kuendeleza kudhibiti uvuvi uliopitiliza kiwango katika maeneo nje ya MCAs kwa kutumia mbinu za PSE, pamoja na kuandaa masharti yatakayosaidia kuzuia uvuvi unaopitiliza kiwango katika maeneo ya bahari ya karibu na pwani, katika kipindi cha muda mrefu. Hatua hizi ambazo zinahusiana na usimamizi wa uvuvi zinaweza kuainishwa kwa ufupi, kama ifuatavyo:

- Kutekeleza na kufuatilia kwa ufanisi mfumo wa usajili na leseni za uvuvi kwa lengo la kumaliza tatizo lililopo la uvuvi huru usiozingatia kanuni.
- Utendaji kazi wa Maeneo ya Hifadhi ya Bahari (MCAs)
- Kutumia mbinu za Kanuni za Kipaumbele cha Kusimamia sheria ipasavyo (PSE) ndani na nje ya Maeneo ya Hifadhi ya Bahari (MCAs).
- Kuanzisha utaratibu wa Mpango wa Uvuvi katika aina za uvuvi zilizoteuliwa, huku kipaumbele kikitolewa katika shughuli zenye lengo la kubadilisha mfumo wa sasa wa utawala wa uvuvi katika aina husika ya uvuvi.

Lengo la Mkakati kwa muda wa kati hadi muda mrefu litakuwa ni kufikia lengo la usimamizi bora wa uvuvi wa bahari ya karibu na pwani kwa kuhakikisha kuwa kunakuwa na uwiano baina ya shughuli za uvuvi zinazofanyika katika eneo la maji madogona kiwango cha rasilimali za bahari zilizopo katika maeneo hayo, na kwa mujibu wa malengo ya usimamizi. Hii ina maana kwamba kuna haja ya kuanzisha **mipango ya maeneo sahihi ya uvuvi kwa kiwango cha uvuvi kinachokubalika** (aina au makundi maalumu ya samaki, aina maalumu za vyombo vya kuvulia, maeneo maalumu ya kuvua – kama Maeneo ya Hifadhi ya Bahari (MCAs) -, ghuba, maeneo ya mito ya bahari, visiwa vidogo n.k.), kwa mashauriano ya karibu na wadau wa uvuvi.

Hatua nyengine zitakazosaidia usimamizi mzuri wa uvuvi, kwa mujibu wa Vision 2020, zitakuwa ni pamoja na:

- Kutumia vizuri mbinu za asili za usimamizi wa uvuvi (kama masimu ya marufuku ya kuvua, na maeneo marufuku ya kuvua);
- Kupanua mtandao wa Maeneo ya Hifadhi ya Bahari (MCAs) (CHABAMCA, TUMCA, and

Kojani in Pemba Island);

- Kufanya marekebisho madogo ya mbinu za kitaalamu za usimamizi wa uvuvi ndani na nje ya MCAs na wakati huo huo kuendelea kuimarisha matumizi ya mbinu za PSE;
- Kufanya majaribio ya matumizi ya matumbawe bandia katika maeneo yanayofaa.

4.5 KUENDELEZA UVUVI WABAHARI KUU

4.5.1 KUENDELEZA MATAYARISHO NA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU YA KUANZISHA NA KUSIMAMIA UVUVI WA FAD

Uanzishaji wa Uvuvi wa kutumia FAD ni lazima ufanywe kwa umakini na wende hatua kwa hatua ili kupunguza hatari za kufeli kwa miradi na kupoteza fedha za umma. Hatua ya kwanza iwe ya maandalizi ya **programu shirikishi ya maendeleo na usimamizi wa uvuvi wa FAD**, kwa mujibu wa misingi elekezi kama ilivyofafanuliwa katika sehemu 3.2.2. Katika maandalizi hayo ya programu, mkazo uwekwe katika vipengele vya kitaalamu (kama mbinu za uvuvi na usafiri wa majini, aina za FAD, matumizi ya FAD kwa mujibu wa mazingira ya eneo la uvuvi n.k.) na uongezaji wa thamani (utunzaji wa samaki chomboni, uhifadhi wa samaki, kuwatayarisha na kuwauza). Aidha, hatua hii ijumuishe kufanyika kwa utafiti wa uvuvi wa FAD na mashauriano kati ya Uongozi wa Uvuvi, taasisi nyengine za umma zinazohusika na mchakato wa maendeleo ya uvuvi wa FAD (Serikali za Maeneo husika, KMKM, DSFA, Wakala wa Elimu na Mafunzo ya uvuvi – Fisheries Education and Training Agency (FETA) –, taasisi za mikopo, n.k.) na wadau wengine wa sekta ya uvuvi. Programu pia iangalia ichukuwe uzoefu kutoka Mkakati wa Usimamizi wa Uvuvi wa Tuna Tanzania wa mwaka 2012[3], ambao unaihusu pia Zanzibar.

Programu hii inapaswa kuwa na vipengele mbali mbali ambavyo ni pamoja na:

- Mkakati wa matumizi ya FAD
- Kuandaa mazingira mazuri ya matumizi wa FAD (kuwajengea uwezo wavuvi, miundombinu, vifaa, huduma za mikopo, Ufuatiliaji Udhibiti na Ulinzi, usalama baharini n.k.)
- Mpango wa Uzalishaji wa FAD
- Mkakati wa matengenezo na ubadilishaji wa FAD
- Ufuatiliaji na Tatmini ya Uvuvi wa FAD (hasa kupima athari za uvuvi wa FAD kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi Zanzibar na katika kupunguza uvuvi unaofanyika katika bahari ya kina kidogo)

Pamoja na ukweli kwamba uanzishaji na usimamizi wa programu ya uvuvi wa FAD utasaidia katika kufikiwa kwa malengo ya kunyanyua uchumi na kuimarisha usalama wa chakula kama ilivyoainishwa kwenye Vision 2020 na MKUZA II, pia utasaidia kwa upande kiasi fulani kuondosha kiwango kikubwa cha uvuvi katika bahari ya kina kifupi na hatimaye kupunguza uharibifu wa mazingira ya miamba ya matumbawe. Hali hii itasaidia pia katika kufikia lengo la kuimarisha usimamizi wa rasilimali za bahari na ukanda wa pwani ili kuendeleza utalii kama ilivyosisitizwa katika Vision 2020.

3 Lengo la jumla la Mkakati wa Usimamizi wa Uvuvi wa Tuna Tanzania ni: “Usimamizi na matumizi endelevu ya tuna na rasilimali (samaki) nyengine zinazohama mara kwa mara ili kuleta tija za kibaiolojia, kimazingira, kijamii na kiuchumi kwa wananchi wa Tanzania”. Lengo la msingi la Mkakati wa Tuna ni kuimarisha Usimamizi wa meli za Nchi Zinazovua katika Bahari za Mbali (Distant Water Fishing Nations – DWFN) zinazofanya kazi katika maeneo ya Ukanda Maalumu wa Kiuchumi (Exclusive Economic Zone – EEZ) kuzuia Uvuvi Haramu, Usiofahamika na Usiofuata Kanuni (Illegal, Unreported and Unregulatory – IUU), kuongeza thamani ya tuna wanaovuliwa, na kuimarisha uanzishaji wa uvuvi tuna kwa kutumia meli za ndani.

4.5.2 KUIMARISHA UFANISI NA USALAMA WA VYOMBO VYA UVUVI KATIKA BAHARI KUU

Baadhi ya vyombo vya uvuvi huvua mbali na pwani katika bahari kuu. Hata hivyo, vyombo hivyo vina kasoro za kitaalamu zinazosababisha kushuka kwa ufanisi wake kiuchumi pamoja na matatizo ya kiusalama baharini. Kuna haja ya kujenga mazingira mazuri yatakayowasaidia wavuvi kupata vyombo vya kisasa vya uvuvi (ikiwemo boti na vifaa vya uvuvi). Kufikiwa kwa lengo hili kunahitaji kwanza kufanyika utafiti tumizi kuhusu teknolojia ya uvuvi, kuanzisha mashirikiano na taasisi za mikopo na kutoa huduma za uenezi (matangazo, ushauri wa kitaalamu, mafunzo n.k.).

Wakati mambo hayo yakitekelezwa, kuna haja ya kufanya tathmini kwa hatua zilizowahi kuchukuliwa huko nyuma ili kujifunza kwa ajili ya hatua za baadaye.

4.6 KUIMARISHA MAENDELEO YA KILIMO CHA BAHARINI KINACHOZINGATIA UHIFADHI WA MAZINGIRA

4.6.1 KUENDELEZA KILIMO CHA MWANI

Ukulima wa mwani umekuwa kwa kiasi kikubwa katika muongo uliopita na kwa sasa ni miongoni mwa shughuli muhimu za kujiongezea kipato kwa jamii za ukanda wa pwani, hasa wanawake. Aidha, zao hili lina nafasi kubwa ya kukua zaidi, lakini linakamiliwa na matatizo ya masoko, hasa bei ndogo kwa wakulima. Kunyanyua thamani ya zao hili kutasaidia kuongeza uzalishaji wake na hatimaye kuchangia katika kupunguza umasikini kwa jamii za pwani. Mambo yanayoweza kuongeza thamani

zao la mwani ni pamoja na kuwapa wakulima nafasi zaidi ya kupatana bei na kuimarisha viwanda vidogo vya usarifu wa mwani Zanzibar, kwa kushirikiana na wawekezaji binafsi.

Zaidi ya hayo, kuna umuhimu mkubwa wa kutilia mkazo masuala ya mazingira kwa sababu kilimo cha mwani kitazidi kukua. Mwisho kabisa, matayarisho ya mipango ya kiasili ya usimamizi wa mazingira ya ukanda wa pwani, kama uwekaji wa zoni (mfano zoni zisozotakiwa kulima mwani) yanaweza kufanyika kwa kushirikiana na Kamati za Mwani za Vijiji (Village Seaweed Fishing Commitees – VSFCs).

4.6.2 KUIMARISHA MATAYARISHO NA UTEKELEZAJI WA MPANGO MKAKATI WA KILIMO CHA BAHARINI ZANZIBAR.

Shughuli nyengine za kilimo cha baharini ni ufugaji wa samaki hasa mwatika (milkfish au chanos chanos) na mkizi (mullet au Mugil sp). Pia katika ukanda wa pwani katika visiwa vya Zanzibar kuna ufugaji wa chaza, kombe, majongoo ya pwani na ukuzaji wa kaa. Aidha, aina nyengine ya samaki ambayo ina uwezekano wa kufugika ni kolekole (Caranx sp). Hata hivyo, shughuli hizi za ufugaji wa samaki bado zipo katika kiwango cha chini sana, kwa hivyo kuna haja ya kuimarisha hatua za kunyanyua maendeleo ya shughuli hizi zenye mwelekeo mzuri kwa siku zijazo.

Maelezo ya hapo juu yanaonesha umuhimu wa Zanzibar kuandaa mpango mkakati wa kilimo cha baharini utakaopelekea kuwepo kwa mazingira mazuri kwa sekta binafsi kuongoza katika kujishughulisha na sekta hiyo ili kuongeza uzalishaji katika kilimo hicho kwa Zanzibar. Mpango mkakati uimarishe kilimo cha baharini cha biashara na ushirikiano kati ya taasisi za umma na sekta binafsi kwa mujibu wa MKUZA II.

Aidha, Mpango mkakati huo ushughulikie matatizo yote ambayo yanakwamisha maendeleo ya sekta ya kilimo cha baharini, ikiwemo suala la uhusiano kati wanunuzi wa wakulima wa mwani, upungufu wa mbegu bora, vifaranga na chakula cha samaki, ukosefu wa mbinu za kitaalamu na usimamizi miongoni mwa wakulima wadogo, matatizo ya upatikanaji wa mikopo ambayo watu wanaojishughulisha na kilimo cha baharini wanaweza kuimudu, kutokuwepo kwa mazingira mazuri ya kisheria na huduma mbaya za uenezi. Pia, mpango mkakati wa kilimo cha baharini unapaswa kubainisha maeneo yanayofaa kutumika kwa shughuli hizo, mfumo wa uzalishaji, na aina za samaki wanaopaswa kufugwa na mwani unaofaa kulimwa. Mwisho, mpango mkakati unapaswa kushughulikia ipasavyo haja ya kuwepo kwa uwiano katika ya kilimo cha baharini na uhifadhi na usimamizi wa mazingira katika ukanda wa pwani.

4.7 KUIMARISHA ONGEZEKO LA THAMANI NA KUSAIDIA KUPUNGUZA UMASIKINI KATIKA SEKTA YA BAADA YA MAVUNO

Kama ilivyoelezwa katika misingi elekezi mikuu za Mkakati, kuimarisha uongezaji wa thamani katika uvuji usiofuata taratibu utaongeza matatizo ya kibaiolojia, kiekiolojia, kijamii na kiuchumi katika uvuvi unaoendelea sasa, ambao kwa kiasi kikubwa umemaliza au kutumia rasilimali zote za baharini katika maeneo ya kina kifupi cha bahari. Endapo matatizo hayo yatatatuliwa katika kipindi cha muda wa kati au muda mrefu, hatua za kuongeza thamani na kupunguza umasikini, kidogo kidogo, zitakuwa ndiyo vipaumbele katika kipindi hicho.

Hatua hizo zinapaswa kubainishwa wazi wazi kwa kufanya uchambuzi wa mlolongo wa thamani (kutoka kwa wavuvi hadi kwa wateja) na tafiti nyengine za kiuchumi, kwa kushirikiana na wadau wa uvuvi, serikali za vijiji, na taasisi nyengine za umma, ambazo kwa namna moja au nyengine zinahusika na shughuli za uvuvi, kama vile Idara ya Ardhi, Wizara ya Biashara, Wizara ya Afya, Bodi ya Chakula na Dawa na Vipodozi Zanzibar (ZFDB), Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA), Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO), Idara ya Ushirika, Idara ya Mazingira na Kamisheni ya Utalii.

Hata hivyo, ni vyema kusisitizwa kwamba hatua yoyote ile, yenye lengo la kupunguza za mazao na kiuchumi baada ya mavuno, na ambayo inakusudia kusaidia kuwepo kwa mgawanyo wa thamani miongoni mwa wadau wa uvuvi na shughuli nyengine zinazohusiana na uvuvi, iwe ni ya muda mfupi hadi muda wa kati. Hatua hiyo ilenge samaki wadogo wanaovuliwa katika bahari kuu.

4.7.1 KUONGEZA UBORA WA SAMAKI PAMOJA NA KUPUNGUZA UPOTEVU WA SAMAKI NA HASARA YA KIUCHUMI

Kuna hatua nyingi za kuongeza ubora wa samaki kwa ajili ya kuwanufaisha wateja wa watu wengine wanaofaidika kiuchumi. Hatua hizi ni pamoja na kuimarisha miundombinu na nyenzo katika masoko katika kusaidia biashara ya samaki na kupunguza upotevu wa samaki, kuimarisha mhimili wa kisheria na kitaasisi kwa madhumuni na kuongeza uwezo wa kudhibiti ubora wa samaki. Hatua nyengine ni kuimarisha tafiti za matumizi na huduma za uenezi, kuongeza uelewa wa namna ya kuwaweka, kuwahifadhi na kuwatayarisha samaki kwa ajili ya kuwauza.

Ni muhimu kuandaliwa kwa ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi kwa ajili ya utekelezaji wa hatua hizo, wakiwemo jamii za wavuvi, wauzaji wa samaki na wawekezaji binafsi.

4.7.2 KUONGEZA THAMANI KATIKA UVUVI (MUDA WA KATI HADI MREFU)

Hatua zenye lengo la kuongeza thamani katika uvuvi na kusaidia kuondoa umasikini zitawekwa wazi kwa mujibu wa uchambuzi wa mlolongo wa thamani katika uvuvi. Miongini mwa hatua zinazopaswa kupewa kipaumbele ni kuimarisha miundombinu na nyenzo katika masoko, kuanzisha mfumo wa taarifa za masoko, kuimarisha utafiti tumizi na huduma za ueneza (kwa mfano tafauti za samaki na mbinu za kuwaandaa samaki kwa ajili ya mauzo, kuongeza uelewa kwa wavuvi na wadau wengine wanaohusika na uvuvi kuhusu namna bora ya kuwashughulikia samaki, kunyanyua bei za samaki na kuimarisha mfumo wa minada ya samaki.

Pia ni muhimu kuwa na mfumo rasmi wa mashirikiano kati ya sekta ya umma na sekta rasmi katika kushajiishana utekelezaji wa hatua hizi. Sekta binafsi ni pamoja na jamii za wavuvi, wauzaji wa samaki, na wawekezaji binafsi.

5. UTEKELEZAJI WAMKAKATI WA UTAWALA WA UVUVI

5.1 UFUPISHO WA MIONGOZO YA UTEKELEZAJI KWA AJILI YA KUIMARISHA UTAWALA NA USIMAMIZI WA UVUVI PAMONA NA HATUA ZINAZOPEWA KIPAUMBELE

Ufupisho wa kila hatua inayopaswa kuchukuliwa katika kila kipengele cha mkakati umeoneshwa katika kiambatisho hapo chini, kwenye mfumo wa jadweli muda wa utekelezaji (**MMK)** ikimaanisha Muda Mfupi hadi wa kati na (**MKM)** ikiwakilisha Muda wa Kati hadi Mrefu). Jadweli hili litasaidia katika kubainisha miongozo ya utekelezaji (ratiba) kwa ajili ya Utekelezaji wa Mkakati wa Utawala wa Uvuvi.

Hatua za kipaumbele ni kama zifuatazo:

- Kuandaa na kupitisha Sera Mpya ya Uvuvi inayoakisi mwongozo huu wa utekelezaji, kwa kuelewa kwamba Sera ya Uvuvi itakuwa ni nyenzo kuu ya kisera itakayosaidia utekelezaji wa Mkakati wa Utawala wa Uvuvi (Angalia 1.1)
- Kuimarisha utawala wa Maeneo ya Hifadhi ya Bahari (MCAs) yaliyopo (Angalia 4.1)
- Kuweka masharti ya chini ya kukubaliwa kuvua, ikiwemo usajili wa vyombo vya uvuvi, leseni kwa vyombo vya uvuvi, wavuvi na watu wengine wanaojishughulisha na kazi zinazowiana na uvuvi (Angalia 3.1)
- Kuimarisha Mfumo wa Ufuatiliaji, Udhibiti na Ulinzi (MCS) kwa kutumia mbinu za Kanuni za Kipaumbele cha Kusimamia sheria ipasavyo (PSE) ndani na nje ya Maeneo ya Hifadhi ya Bahari (MCAs) (Angalia 1.2, 2.2, na 4.2)
- Kusaidia uandaaji na usimamizi wa Uvuvi shirikishi wa kutumia Maumbo Yanayowavutia Samaki (FAD) (Angalia 3.2.2)
- Kuanzisha haraka iwezekanavyo utaratibu wa kuimarisha takwimu na mfumo bora wa utafiti (Angalia 2.1 na 2.3)

5.2 BAADHI YA MISINGI ELEKEZI YA UTEKELEZAJI WA MKAKATI WA UTAWALA WA UVUVI

Kuchukua hatua na kutumia fursa zilizopo

Katika hali ya sasa ambapo kuna matatizo ya kibajeti na ukosefu wa nguvu kazi ya kutosha ni muhimu kubadiliko kulingana na hali ilivyo na kutumia fursa zilizopo katika utekelezaji wa Mkakati wa Utawala wa Uvuvi. Mkakati unaelekeza kufuatwa kwa misingi elekezi na inapendekeza miongozo ya utekelezaji kwa ajili ya kuimarisha utawala na usimamizi wa uvuvi. Pamoja na kwamba baadhi ya vipengele hivi havifikii kikamilifu masharti na vipaumbele vya washirika wa maendeleo, hicho kisiwe kikwazo cha kupata misaada kwa sababu suala la uimarishaji wa utawala na usimamizi wa uvuvi ni jambo linalokwenda hatua kwa hatua na linalohitaji kubadilika kwa mujibu wa hali halisi ilivyo.

Vile vile, inapindekezwa kwamba vipengele vya mikakati vilivyotajwa katika Mkakati wa Utawala wa Uvuvi vizingatiwe wakati wa majadiliano kati ya Serikali na washirika wa maendeleo.

Ufuatiliaji na Tathmini

Ufuatiliaji na Tathmini ni nyenzo muhimu sana inayosaidia utekelezaji wa Mkakati wa Utawala wa Uvuvi na husaidia katika majadiliano kati ya sekta ya umma na wadau binafsi ambao kwa namna moja au mwengine wanahusika na usimamizi na maendeleo ya uvuvi.

Ni vyema kulifafanua zaidi jadweli linalooneshwa katika kiambatisho kwa kutafuta viashiria sahili vinavyopimika kwa urahisi. Hilo linaweza kufanyika katika kikao maalumu cha wadau mbali mbali wa uvuvi.

Ushirikiano

Utekelezaji wa Mkakati wa Utawala wa Uvuvi unaelekeza kuwepo kwa ushirikishwaji wa taasisi mbali mbali za umma na binafsi ambazo kwa namna moja au nyengine zinahusika na masuala ya uvuvi, huku Uongozi wa Uvuvi ukiwa taasisi itakayoongoza katika utekelezaji, ufuatiliajina tathmini ya Mkakati huo. Uongozi wa uvuvi pia utakuwa na kazi ya kuchochea utekelezaji wa Mkakati.

Katika muktadha huo, ushirikiano wa karibu na taasisi za umma na binafsi zifuatazo unapaswa kuendelezwa:

Taasisi za Umma

- Taasisi za Kitaaluma za Utafiti: IMS, SUZA, ZU (Zanzibar University)
- Serikali za Mikoa
- Idara ya Ushirika
- Mamlaka ya Usimamizi wa Uvuvi katika Bahari Kuu (Deep Sea Fishing Authority – DSFA)
- Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar (ZMA)
- Kikosi Maalumu cha Kuzuia Magendo (KMKM)
- Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP)
- Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG)
- Wizara ya Mazingira
- Wizara ya Misitu
- Kamisheni ya Utalii
- Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar (ZFDB)
- Taasis ya Viwango Zanzibar (Zanzibar Bureau of Standards – ZBS)
- Idara ya Maafa
- Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA)
- Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO)
- Idara ya Ardhi
- Mamlaka ya Bandari
- Wizara ya Mawasiliano
- Wizara ya Fedha
- Wizara ya Afya, Chuo cha Afya
- Wizara ya Biashara
- Kamisheni ya Utumishi wa Umma
- Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (Office of Chief Government Statistics – OCGS)

Taasisi Binafsi

- Sekta binafsi na wawekezaji
- Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs)
- Kamati za Uvuvi za Vijiji (VFCs)

- Jumuiya ya Wakulima wa Mwani Zanzibar (ZASEFA)
- Ushirika wa Kuendeleza Makasha ya Mapambo (CHAZA)

Nyengine

- Taasisi Zinazotoa Mikopo: Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), Mamlaka ya Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA)
- Vyombo vya Habari
- Jumuiya ya Wafanyabiashara, Wenyeviwanda na Wakulima Zanzibar (Zanzibar National Chamber of Commerce Industry and Agriculture – ZNCCIA)

6. KIAMBATISHO: BANGO KITITA LA MKAKATI WA KUIMARISHA UTAWALA NA USIMAMIZI WA UVUVI ZANZIBAR

MIPANGO YA MKAMKATI (MIKUU NA MIDOGO	MUDA WA UTEKELEZAJI		HATUA NA/AU MAELEZO
	MMK	MKM	
1. Kuimarisha vipengele muhimu vya mhimili wa utawala wa uvuvi			
1.1 Kuipitia na kuifanyia marekebisho Sera ya Uvuvi ya mwaka 2000	X	--	Nyenzo kuu ya sera ya utekelezaji wa Mkakati
1.2 Kushajiisha Ukamilishaji na Upitishaji wa Vifungu vya sheria ya Uvuvi ya mwaka 2010 vinavyosaidia utekelezaji wa Mkakati	X	--	• Kanuni za Ufuatiliaji, Udhibiti na Ulinzi (MCS) • Kanuni za uvuvi (kwa mujibu wa Kanuni ya Kipaumbele cha Kusimamia sheria ipasavyo (PSE).
1.3 Kuimarisha Ufanisi katika Uongozi wa Uvuvi	X	X	• Kufanya mabadiliko madogo ya kitaasisi katika ngazi ya kitaifa • Mafunzo ya usimamizi wa uvuvi • Kujenga uwezo katika uongozi wa maeneo ya uvuvi • Kupeana taarifa miongoni mwa taasisi mbali mbali
1.4 Kuzijengea uwezo taasisi za uvuvi za kijamii na binafsi	X	X	• Kujenga uwezo kwa Kamati za uvuvi za Kijiji (VFCs) • Mfumo wa mashauriano miongoni mwa Kamati za Uvuvi Za Vijiji (katika maeneo yao ya usimamizi) • Kuanzisha jumuiya ya kitaifa ya wavuvi

MIPANGO YA MKAMKATI (MIKUU NA MIDOGO	MUDA WA UTEKELEZAJI		HATUA NA/AU MAELEZO
	MMK	MKM	
1.5 Kuimarisha ushirika wa Uvuvi wa kimataifa, kikanda na kitaifa	X	X	• Kuongeza ushiriki wa wawakilishi wa Zanzibar katika ushirika wa uvuvi wa kimataifa na kikanda • Kuufanya mfumo wa ushirikiano kati ya Tanzania Bara na Muungano kuwa rasmi (ushirikiano wa kitaalmu na kisayansi) • Kuanzisha kamisheni ya mashauriano ya pande mbili na Tanzania Bara (kuoanisha kanuni na usimamizi wa uvuvi unaomilikiwa na pande zote kwa pamoja)
1.6 Kufanya marekebisho ya Sheria ya Uvuvi ya mwaka 2010 kwa lengo la kuimarisha utawala wa uvuvi	--	X	Sheria zianzishwe au ziendelezwe: Bodi ya udhamini, mfumo wa taarifa, ppp, Mfuko wa usimamizi wa uvuvi
2. Kuimarisha utoaji wa huduma muhimu za uvuvi			
2.1 Kuufanyia marekebisho mfumo wa takwimu na taarifa	X	X	Ukusanyaji wa data, taratibu za ukusanyaji na utoaji wa data, kuchapisha taarifa za kila mwaka
2.2 Kuendelea kuimarisha Ufuatiliaji, Udhibiti na Ulinzi katika uvuvi (MCS)	X	X	• Kuimarisha kitengo cha MCS (kifedha na kiuhuru wa utendaji) • Mfumo wa ushirikiano na KMKM, DSFA, MCS ya Tanzania Bara, Polisi Zanzibar na Mfumo wa mahakama • Kuongeza nyenzo za utendaji wa kila siku • Kuimarisha mpango wa utendaji (Maeneo ya Hifadhi ya Bahari, Kanuni ya Kipaumbele cha Kusimamia sheria ipasavyo , mfumo wa taarifa za kipepelezi)
2.3 Kuanzisha mfumo bora wa utafiti wa uvuvi	X	X	• Kuimarisha uwezo wa kitengo cha Utafiti cha WMU (ikiwemo kuajiri mratibu wa uvuvi kwa ajili ya Kamati ya Kitaalamu ya Uvuvi • Mkataba wa Mahirikiano (MoU) kuhusu kupeana data kati ya Kitengo cha Utafiti na Uongozi wa uvuvi • Mpango wa mafunzo kwa watafiti (Ikiwemo SUZA, IMS, na ZU) • Programu za kisayansi (zitakazohusisha taasisi za umma na binafsi) • Kufanya warsha ya kisayansi kila baada miaka 4 au 5 • Mawasiliano ya kisayansi

MIPANGO YA MKAMKATI (MIKUU NA MIDOGO	MUDA WA UTEKELEZAJI		HATUA NA/AU MAELEZO
	MMK	MKM	
2.4 Kuanzisha mfumo wa taarifa za uvuvi	--	X	*Mfumo wa mawasiliano unapaswa kuhusisha moduli 3: 1. Mhimili wa usimamizi wa uvuvi 2. Hali ya Sekta ya Uvuvi 3. Maendeleo ya sekta ya uvuvi*
2.5 Ufuatiliaji na Tathmini ya Mkakati	X	X	• Mfumo wa ufuatiliaji na tathmini za mara kwa mara • Mkutano wa wadau mbali mbali baada ya kila miaka 3
3. Kuufanya uvuvi na kazi nyengine zinazohusiana na uvuvi kuwa rasmi na za kitaalamu			
3.1 Kuweka masharti ya chini ya kukubaliwa kuvua	X	X	• Usajili wa vyombo vya uvuvi • Leseni za vyombo vya uvuvi • Leseni kwa wavuvi na wengine wenye kazi zinazohusiana na uvuvi *Kutoa taarifa za uvuvi kwa wavuvi na watu wengine wanaofanya kazi zinazohusiana na uvuvi, kuongeza uelewa wa masualaya leseni kwa maafisa uvuvi wa Wilaya (District fisheries Officers (DFOs). Kuwa na data za usajili na leseni zilizohifadhiwa katika kompyuta katika kiwango cha Idara ya Uvuvi (DFD), kujaribu mfumo wa usajili na leseni wa kutumia simu za mkononi.*
3.2 Kumalizia uanzishaji wa madiko rasmi	---	X	
3.3 Kuimarisha hali ya maisha ya jamii za wavuvi (mkazo ukiwa kwa vijana)	X	X	• Kuwa na wavuvi walioelimika na wa kisasa • Ushirikishwaji mzuri wa jamii za wavuvi katika programu za kijamii. • Utatuzi wa migogoro katika uvuvi • Kuimarisha mkakati wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi
4. Kuimarisha usimamizi wa uvuvi wa karibu na pwani			
4.1 Kufanya kazi na kuimarika kwa usimamizi wa Maeneo ya Hifadhi ya bahari	X	X	• (Kukamilisha/kupitisha mswada wa kanuni za Kitengo cha Hifadhi ya Bahari – MCU) • Kuimarisha uwezo wa MCU • Kuifanyia mabadiliko na kuipitisha Mipango Mikuu ya Usimamizi (GMPs) iliyopo ya Maeneo ya Hifadhi ya Bahari – MCAs (kwa mujibu wa PSE)

MIPANGO YA MKAMKATI (MIKUU NA MIDOGO	MUDA WA UTEKELEZAJI		HATUA NA/AU MAELEZO
	MMK	MKM	
4.2 Kuimarisha Mbinu za Kipaumbele cha Kusimamia sheria ipasavyo (PSE) kwa Maeneo yaliyo nje ya MCAs	X	X	• Kuchora ramani ya kuainisha maeneo ya uvuvi (kuainisha maeneo nyeti ambayo yatapigwa marufuku uvuvi wa kutanda karibu na fukwe) • Kutoa orodha ya mwisho ya kanuni za kipaumbele kwa mashauriano na wavuvi • Kushauriana na kuongeza uelewa na wavuvi na wengine wenye kazi zinazohusiana na uvuvi kuhusu PSE • Adhabu zinazofaa kwa ajili ya watakaovunja kanuni za kipaumbele (na kuzifanya ziwe kanuni za uvuvi) • Kuweka utaratibu wa utekelezaji wa MCS • Kuongeza uelewa kwa serikali za mitaa na uongozi wa maeneo • Taarifa na mawasiliano ya mara kwa mara kuhusu utekelezaji wa PSE
4.3 Kuimarisha Mipango ya Usimamizi wa Uvuvi katika aina za Uvuvi zilizotuliwa	X	X	• Kutafuta Mipango ya Usimamizi wa Uvuvi (FMPs) inayopaswa kupewa kipaumbele (kwa mujibu wa makubaliano ya pamoja ya kitengocha usimamizi wa uvuvi) • Kuzindua mchakato wa Mipango ya Usimamizi wa Uvuvi katika aina za uvuvi zilizoteuliwa kupewa kipaumbele (aina za usimamizi, mabadiliko ya kitaasisi, hatua za haraka za usimamizi) • Kutekeleza (na kufanyia marekebisho) Mipango ya Usimamizi wa Uvuvi –FMPs)
4.4 Kuendeleza utekelezaji wa hatua za Usimamizi Shirikishi wa Ukanda wa Pwani (ICZM)	X	X	• Utekelezaji wa Usimamizi Shirikishi wa Ukanda wa Pwani (ICZM) kwa kuimarisha ushirikiano wa taasisi mbali mbali • Kulenga katika kulinda mazingira (kwa mfano mikoko na majani ya baharini, kutia dawa mfumo wa michirizi ya maji machafu, kusimamia sheria za mazingira) • Kuongeza uelewa kwa jamii zinazoishi maeneo ya ukanda wa pwani ndani na nje ya Maeneo ya Hifadhi ya Bahari (MCAs)
4.5 Kuimarisha mfumo wa kitaifa wa kulinda na kupambana na uchafuzi wa mazingira ya bahari	X	X	• Kutekeleza mfumo wa kitaifa wa kulinda na kupambana na uchafuzi wa mazingira ya bahari (Marine Pollution – MARPOL) • Kutoa kipaumbele kwa Maeneo ya Hifadhi ya Bahari (MCAs)

MIPANGO YA MKAMKATI (MIKUU NA MIDOGO	MUDA WA UTEKELEZAJI		HATUA NA/AU MAELEZO
	MMK	MKM	
4.6 Kuimarisha usimamizi wa uvuvi wa maeneo ya karibu na pwani	X	X	• Kuanzisha mipango ya maeneo yanayofaa kwa uvuvi katika kiwango kinachofaa zaidi • Kuongeza mtandao wa Maeneo ya Hifadhi ya Bahari (CHABAMCA, TUMCA, na Kojani) • Kufanya mabadiliko madogo ya hatua za usimamizi ndani na nje ya Maeneo ya Hifadhi ya Bahari huku mbinu za PSE zikiimarishwa • Kufanya majaribio ya matumbawe bandia katika maeneo yanayofaa *Masharti ya kufanikiwa: mfumo mzuri wa usajili na leseni (kuacha mfumo wa uvuvi huru na ambao kwa kiasi kikubwa ni bure), utendaji kazi wa Maeneo ya Hifadhi ya Bahari (MCA) yaliyopo, matumizi ya PSE ndani na nje ya MCA, Kuendelea na utaratibu wa Mipango ya Usimamizi wa Uvuvi wa kuteuwa aina za uvuvi zinazopaswa kupewa kipaumbele*
5. Kuimarisha uvuvi kwa wavuvi wadogo katika Bahari Kuu			
5.1 Kuimarisha maendeleo na usimamizi wa uvuvi shirikishi wa kutumia Maumbo Yanayowavutia Samaki (FAD)	X	X	• Kutayarisha programu shirikishi ya uvuvi wa FAD ikiwemo kufanya majaribio ya namna Maumbo Yanayowavutia Samaki na mbinu zinazotumika vinaweza kuoana na mazingira yanayotumika, kwa ushirikiano na wavuvi • Kutekeleza programu ya maendeleo na usimamizi wa uvuvi shirikishi wa kutumia Maumbo Yanayowavutia Samaki (FAD) *Programu hii iwe na vipengele vitano (5): Mkakati wa matumizi ya FAD, Mazingira mazuri kwa ajili ya maendeleo ya uvuvi wa FAD, Mpango wa utumiaji wa FAD, Mkakati wa kutengeneza na kubadilisha FAD, Kufuatilia na Kutathmini uvuvi wa FAD*

MIPANGO YA MKAMKATI (MIKUU NA MIDOGO	MUDA WA UTEKELEZAJI		HATUA NA/AU MAELEZO
	MMK	MKM	
5.2 Kuimarisha ufanisi na usalama baharini kwa vyombo vinavyovua mbali na pwani	X	X	• Kufanya tathmini kwa hatua zilizochukuliwa hapo awali ili kujifunza wakati wa kubainisha hatua za kuchukua baadaye • Matumizi ya utafiti katika teknolojia ya uvuvi • Mashirikiano na taasisi za mikopo • Huduma za uenezi (matangazo, ushauri wa kitaalamu, mafunzo n.k.)
6. Kuimarisha maendeleo ya kilimo cha baharini kinachozingatia uhifadhi wa mazingira			
6.1 Kuendeleza kilimo cha mwani	X	X	• Kuongeza thamani kwa mzalishaji (kuongeza bei ya mwani) • Kuendeleza viwanda vidogo vya kutayarisha mwani • Kutayarisha mipango ya usimamizi wa ukanda wa pwani kwa maeneo husika, ikiwemo kuweka zoni maalumu za kulimia mwani
6.2 Kuimarisha Mkakati wa Kilimo cha baharini Zanzibar (na aina nyengine kilimo cha baharini)	X	X	• Kuangalia mradi wa FAO ambao unaandaliwa kwa ajili ya kutayarisha Mpango Mkakati wa kilimo cha baharini • Kutekeleza Mpango Mkakati wa kilimo cha baharini *Kuweka mkazo katika kuimarisha kilimo cha baharini cha biashara na PPP na kuhakikisha kwamba kuna uwiano kati ya kilimo cha baharini na uhifadhi wa mazingira ya ukanda wa pwani*
7. Kuimarisha uongezekaji wa thamani na kusaidiakuondosha umasikini kwa sekta ya mazao yaliyokwishavunwa			
7.1 Kunyanyua ubora wa samaki ikiwemo kupunguza hasara za upotevu wa samaki na kiuchumi	X	X	• Kuimarisha miundombinu na nyenzo • Kuimarisha mhimili wa kisheria na kiitaasisi katika kudhibiti ubora wa samaki • Kuongeza uelewa kwa wavuvi na watu wengine wanaofanya kazi zinazohusiana na uvuvi • Kuweka vichocheo vya kuimarisha shughuli za kuwabeba, kuwahifadhi na kuwatengeneza samaki *Mkazo uwekwe katika kupunguza hasara za upotevu wa samaki na kiuchumi hasa kwa samaki wadogo wadogo.* *PPP isisitizwe kwa utaratibu maalumu*

MIPANGO YA MKAMKATI (MIKUU NA MIDOGO	MUDA WA UTEKELEZAJI		HATUA NA/AU MAELEZO
	MMK	MKM	
7.2 Kuimarisha ongezeko la thamani katika uvuvi	X	X	• Kufanya uchambuzi wa mlolongo wa thamani kwa lengo la kuchagua programu maalumu • Kutekeleza programu maalumu zenye hatua za kushughulikia miundombinu na nyenzo, mfumo wa taarifa za masoko, tafiti za matumizi na uenezi (kwa mfano mtawanyiko wa bidhaa za samaki na mbinu za utayarishaji wa samaki), kunyanyua bei ya samaki, kuimarisha mfumo wa minada ya samaki n.k. Masharti ya awali: uvuvi udhibitiwe ipasavyo Mkazo uwekwe kuhakikisha kuna mgawanyo mzuri wa thamani inayoongezeka miongoni mwa wavuvi na watu wengine wanaofanya kazi zinazohusiana na uvuvi, kwa kuzingatia tafauti za kijinsia *PPP isisitizwe kwa utaratibu maalumu*